Children in Crossfire



# KITITA cha Matibabu Sanaa na Michezo

# MALENGO ya MABADILIKO

**Children in Crossfire (CiC) ina dhamira ya kulinda na kukuza haki za watoto wanaoishi katika hali ya umasikini.**

Tunakusudia kuweka mazingira salama ambapo yatamwezesha kila mtoto kupata haki zake ikiwa ni pamoja na kuendelezwa ili aweze kufikia ukamilifu wa uwezo wake.

Kwa kuboresha huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto, tunawawezesha watoto na jamii kwa ujumla kujijengea maisha bora ya baadaye.

Kuna maeneo matatu muhimu katika ya dhima yetu ambayo yamezingatia haki za binadamu, mkakati mkabala ili kukidhi mahitaji ya watoto wadogo walioko katika nchi zinazoendelea, kwa kutambua taasisi na mashirika ya kiraia ambayo tunafanya kazi pamoja kwa kuyajengea uwezo ili yaweze:

- Kukabiliana na masuala yote yanayoathri maisha ya totono.
- Kuboresha mazingira wanaishi watoto.
- Kushawishi mabadiliko ya sera zinazohusiana na umasiki unaowabiri watoto


***Shukrani:***

Kitita cha Matibabu Sanaa na Michezo ni matokeo ya shughuli zilizofanyika wakati wa mradi wa majaribio wa Matibabu Sanaa na Michezo katika taasisi ya saratani ya Ocean Road, unaofadhiliwa na kutekelezwa na Children in crossfire (CIC) Tanzania, kati ya Januari na Aprili 2010. Tunapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Taraneh Erfan King kwa kuchua jukumu na nia yake njema ya kufanyakazi na watoto wanaopata matibabu katika taasis hiyo - Haya ndiyo yaliyowezesha maudhui ya kitita hiki cha Matibabu Sanaa na Michezo kufanikishwa. Pia tunamshukuru Tanja Kisslinger (MoyaMaya Media) kwa ajili ya msaada wake wa mawazo na ubunifu pamoja na wafanyakazi wote wa CIC Tanzania na Ireland kwa kuendelea kuuwezesha mradi huu. Shukrani za pekee ziwaendee serikari ya Ireland kupitia mfuko wake wa misaada (Irish Aid) kwa kusaidia kazi za CIC Tanzania, ambapo kitita hiki ni sehemu ya misaada hiyo.



© 2010 Children in Crossfire



Imejumuhishwa na King Taraneh Erfan (MA, Certified Expressive Arts Therapist)
Kazi hii imeboreshwa & kupangiliwa na Tanja Kisslinger (MoyoMaya Media)



**Children in Crossfire**

2 St. Josephs Avenue, Derry / Londonderry
BT48 6TH Northern Ireland
+44 (0)28 7126 9898

P.O. Box 23204
Dar es Salaam, Tanzania
+255 (0)22 277 5965

**infotz@childrenincrossfire.org**
**www.childrenincrossfire.org**

# Utangulizi

## Kitita hiki ni nini?

Children in Crossfire (CiC) imetengeneza kitita hiki kwa matumizi ya walimu wanaofundisha watoto walioko kwenye mradi wa elimu katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI). Shughuli za kila siku za mradi zinahusisha utoaji wa elimu isiyo rasmi pomoja na ubunifu ikiwa ni sehemu ya matibabu kwa watoto wenaumwa saratani na wanaoendelea na matibabu. Kitita hiki kimeandaliwa kwa ajili ya matumizi ya tiba kupitia sanaa na michezo inayofanywa na watoto wenyewe na kinawapatia walimu michezo na shughuli mbalimbali za kufanya wakati wa kuandaa mpango wa mafunzo.

Kutokana na watoto wanaouhudhuria shule/darasani kubabadilika kila siku, ikiwa ni pamoja na tofauti za kiwango cha elimu, umri na utamaduni, kitita kina michezo tofauti tofauti ambayo inawasaidia walimu kuchagua shughuli ambazo zinaendana na hali ya kiafya ya watoto waliopo siku hiyo.

Kwa ujumla kitita kinatoa marejeo stahiki ambayo walimu wanaweza kutumia kupanga kazi zao za kila siku, wakati wote wanapotekeleza malengo yao ya kila siku bila kuwa na mtizamo finyu, kuwapa nafasi watoto kufanya vitu wanavyobuni wenyewe, na kuwajengea hamasa na kujiamini.

## Usisahau Kitini...

Azma ya kitita hiki iko katika sehemu mbili: kuonyesha muktadha na utangulizi juu ya kitita chenyewe na vile vile kuonyesha kwa vitendo miongozo ya utekelezaji wa michezo na shughuli zilizoanishwa kwenye kitita.

Kitita hiki kinatoa utangulizi juu ya umuhimu wa kufanya shughuli mbalimbali na watoto waliothiriwa na saratani katika taasisi ya kansa (ORCI), kazi na umuhimu wa michezo inayohusisha sanaa na vitendo, pamoja na maelezo ya uwezeshaji.

## YALIYOMO

Namna ya kutumia Kitini........................ 4

Kielelezo cha kazi na michezo................ 5

SHUGHULI ZINAZOZINGATIA MICHEZO:

▶ Jina na Kitendo.................................. 6
▶ Rusha mpira....................................... 7
▶ Tembea huku...................................... 8
▶ Mchezo wa wanyama.......................... 9
▶ Chini ya kamba.................................. 10
▶ Pitisha puto....................................... 11
▶ Ingia ndani ya duara.......................... 12
▶ Imba nyimbo ndefu ........................... 13
▶ Rafiki nisaidie kutafuta....................... 14
▶ Kuchanganya changanya..................... 15
▶ Napeleleza na jicho langu dogo.......... 16
▶ Wa kwanza kushika............................ 17
▶ Sepetu................................................ 18
▶ Nataka cha kwangu............................ 19
▶ Kupita kwenye pete mduara............... 20
▶ Bata bukini......................................... 21
▶ Nifuate............................................... 22
▶ Fikiria kitu......................................... 23
▶ Hallo kwa heri.................................. 24
▶ Mtandao wa msaada.......................... 25

SHUGHULI ZINAZOZINGATIA SANAA:

▶ Ninachokiita nyumbani........................26
▶ Paka rangi dunia yangu.......................27
▶ Simulizi hadithi.................................. 28
▶ Kujenga urafiki................................... 29
▶ Mimi na mkono wangu....................... 30
▶ Kuchora ndoto.....................................31
▶ Kama ningekuwa mnyama...................32
▶ Nyumba au nyumbani..........................33
▶ Karibu mgeni.......................................34
▶ Kwenda safari......................................35
▶ Sehemu sita za kisa mkasa................ 36
▶ Mti wa familia.....................................37
▶ Mjumbe mwenye manyoya.................38

## Namna ya kutumia kitita...

**Njia bora ya kutumia kitita hiki ni kujenga uelewa wa shughuli zilizoanishwa kwa kupitia uzoefu wa kutumia kitita.**

**Kama unafanya kazi na wasaidizi, unaweza kusoma na kujadili mada na vitendo vyake kabla au hata kujaribu ukiwa peke yako.**

**Kupanga kazi za siku, kwanza angalia vitu vifuatavyo:**

- Ukubwa wa kundi
- Umri wa wanakikundi
- Nguvu inayotakiwa (kidogo, kiasi, nyingi)

Vile vile unaweza kuzingatia:

- Uwezo wa kimaumbile wa wanakikundikwa mfano: Kuna watoto ambao hawawezi kusimama au kutembea? Kuna watoto ambao hawawezi kuongea au kuona?)
- Hali ya kihisia katika kikundi (kwa mfano, kuna tukio lolote la kusikitisha au la kuvuta hisia ambalo limetokea karibuni na linaweza kuathiri watoto? Inaweza kuwa ni tukio la kawaida kama, kupewa dawa za saratani au kuthoofika kwa mwili/kukosa nguvu au tukio kubwa kama kifo cha mtoto wodini).

**Kwa kuzingatia vipengele vya hapo juu unaweza sasa kuchagua aina ya shughuli zinazofaa kwa siku hiyo.**

Jaribu kuchanganya aina mbali mbali za shughuli, kwa mfano, katika siku mojawapo unaweza kufanya shughuli zifuatazo:

**(1)** Mchezo wa kuchangamsha kuunganisha wanakikundi wenye, (Nguvu ya wastani, kutembea).

**(2)** Mchezo wenye lengo la kuelimisha (kwa mfano kufundisha rangi).


**(3)** Vipindi vya kusimulia hadithi (vikifuatiwa na maelezo mafupi juu ya somo, dhana, picha na wahusika walioshiriki - ambayo yanaweza kulenga tiba ya sanaa au elimu)

**(4)** Shughuli ya kuovyesha picha ikiwa ni mfulululizo wa simulizi ya hadithi, kwa kutumia picha za hadithi/dhana.

**(5)** Majadiliano katika kikundi.

**Jedwali lilopo ukurasa unaofuata linaweza kukusaidia kuchangua shughuli inayofaa kwa siku hiyo** ▶ ▶ ▶ ▶ ▶





## Shughuli zinazozingatia michezo

| Jina la mchezo | Ukubwa wa kundi | Umri | Nguvu inayohitajika |
|---|---|---|---|
| Jina na Kitendo | Kundi dogo/Kubwa | 2+ | Ndogo-Kati |
| Rusha mpira | Kubwa | 5+ | Ndogo-Kati |
| Tembea huku na kule | Kubwa | 3+ | Wastani-Kubwa |
| Mchezo wa wanyama | Kubwa | 4+ | Wastani-Kubwa |
| Chini ya kamba | Kundi dogo/Kubwa | 5+ | Wastani-Kubwa |
| Pitisha puto | Kati/Kubwa | 4+ | Wastani-Kubwa |
| Ingia ndani ya duara | Dogo/Kubwa | 4+ | Ndogo |
| Imba nyimbo ndefu | Dogo/Kubwa | 2+ | Ndogo-Kubwa |
| Rafiki nisaidie kutafuta | Wawili wawili | 6+ | Ndogo-Kati |
| Kuchanganya changanya | Kubwa | 4+ | Wastani |
| Napeleleza na jicho langu dogo | Kubwa | 5+ | Ndogo |
| Wa kwanza kushika | Kubwa | 5+ | Ndogo-Kubwa |
| Sepetu | Kubwa | 8+ | Kubwa |
| Nataka cha kwangu | Kubwa | 6+ | Ndogo |
| Kupita kwenye pete mduara | Kati/Kubwa | 4+ | Wastani |
| Bata bukini | Kati/Kubwa | 2-6 | |
| Nifuate | Kwa vikundi | 3+ | |
| Fikiria kitu | Ndogo/Kubwa | 5+ | |
| Hallo kwa heri | Kubwa | 6+ | Wastani-Kubwa |
| Mtandao wa msada | Kubwa | 5+ | Ndogo |

## Shughuli zinazozingatia sanaa

| Jina la mchezo | Ukubwa wa kundi | Umri |
|---|---|---|
| Ninachokiita nyumbani | Mmoja mmoja au kikundi kidogo | 5+ |
| Paka rangi dunia yangu | Mmoja mmoja au kundi kubwa | 4+ |
| Simulizi hadithi | Dogo au kubwa | 2+ |
| Kujenga urafiki | Kubwa | 4+ |
| Mimi na mkono wangu | Dogo na kubwa | 3+ |
| Kuchora ndoto | Mmoja mmoja au kikundi kidogo | 5+ |
| Kama ningekuwa mnyama | Mmoja mmoja au kikundi | 4+ |
| Nyumba au nyumbani | Kubwa | 6+ |
| Karibu mgeni | Mmoja mmoja au kikundi kikubwa | 5+ |
| Kwenda safari | Kundi kubwa au la kati | 4+ |
| Sehemu sita za kisa mkasa | Mmoja mmoja au kikundi kikubwa | 7+ |
| Mti wa familia | Mmoja mmoja | 6+ |
| Mjumbe mwenye manyoya | | |



## Mchezo # 1: Jina na kitendo

kundi dogo au kubwa / umri 2+ / nguvu ndogo au ya kati

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto kushirikiki kwa pamoja katika mchezo wa kusogea.

Kutoa nafasi kwa wawezeshaji kujua majina ya watoto.

Nia: Kuwapa nafasi watoto kuchagua wenyewe namna watakavyosogea bila kuwachagulia namna ya kusogea, hii inasaidia watoto kuchagua namna ya kusogea ambayo inaendana na uwezo na matumizi nguvu inayoendana na hali yao. Pia inapunguza uwezekano wa watoto kujisikia kwamba hawawezi kufanya chochote hata kama mchezo utakuwa rahisi.

**Vifaa:** Hakuna

**Hatua kwa hatua:**

Wawezeshaji na watoto wasimame kwenye duara.

Kwa kuanza na mwezeshaji kila mmoja ataje jina lake na kufanya kitendo- kwa mfano kuruka juu, kunyanyua mikono, kutetemesha mwili. Kitendo kinaweza kuwa rahisi kama kusogea katikati ya duara.

Waulize wanakikundi kurudia jina la mtu aliyetaja jina lake na kufanya kitendo kwa kadri wanyoweza.

Endelea mpaka kila mmoja aseme jina lake na kufanya kitendo.

**Maelezo kwa mwezeshaji:**

Mara zote kuwa wa kwanza kufanya kitendo ili uonyeshe mfano. Usheshi, ubunifu wa mfano wako utawafanya watoto wawe huru kuonyesha ubunifu wao.

Ni kawaida kwa watoto kurudia vitendo walivyoona watu wengine wakifanya (km Hawabuni kitendo wao wenyewe). Jaribu kuwatia moyo watoto wawe wabunifu na waondoe wasi wasi kwamba hakuna aliye sahihi au mwenye makosa.

**Utofauti katika mchezo:**

Rudia kitendo kama mwanzo ila wakati huu toa maelekezo maalumu juu ya kitendo wanachotakiwa kufanya. Kama vile:

Kitu anachokipenda au mchezo,

Mnyama anayempenda

Unajisikiaje leo (waulize baada ya wiki chache tangu watoto waujue mchezo na kikundi kwa kuwa kufahamu hisia kati yao kunaweza kuleta hofu kati)

Tofauti nyingine katika mchezo huu ni kuweka kitu katikati ya duara. Rudia kitendo kama kawaida ila kwa sasa mpe kila mmoja kitu ulichoweka kwenye duara (kwa mfano; skafu, mpira, mto au kipande cha karatasi) ambacho kundi linaweza kutumia kurushiana. ANGALIZO: Hii inafaa zaidi kwa watoto wakubwa.

### Sababu za kundi/watoto kufurahia mchezo huu...

- ▶ Ni rahisi mwezeshaji kutoa maelezo kwa kutumia mifano.
- ▶ Unaeleweka na watoto wanaoupenda. Watoto wanahamasika na kucheka.
- ▶ Hakuna kiwango cha kitendo "kizuri" na kuna uwekano mdogo wa kukosea (Hii inaweza kutokea tu iwapo kitendo sio kizuri au kinaudhi/kudhalilisha).



# Mchezo # 2: Rusha mpira

## kundi kubwa / umri 5+ / nguvu ndogo – nguvu ya kati

**Lengo:** Kuwahusisha watoto kwenye mchezo wa kuchangamsha au kuamsha mfumo wa fahamu na kumbukumbu.

**Nia:** Mchezo huu unatoa nafasi kwa watoto/kikundi kucheza kwa pamoja na kujengo umoja kati yao. Inafurahisha kuona namna ambavyo watoto wanasaidiana na wanavyo kumbushana namna mchezo unavyoenda na namna wanavyoshikiana kuharakisha mchezo.

**Vifaa:** Mpira mdogo au kifaa laini cha kurusha.

**Hatua kwa hatua:**

Mwezeshaji na watoto wasimame kwenye duara.

Kwa kuanza mwezeshaji arushe mpira kwa mmoja wa wanakikundi ambaye pia atarusha mpira kwa mwanakikundi wa tatu. Kwa mfano, Mary rusha kwa Hassani na Hassani kwa Erene.

Waeleze watoto kwamba lazima wakumbuke mtu anayewarushishia na kwamba watapokea na kurusha kwa watu hao.

Endelea kurusha mpira mpaka kila mmoja awe amerusha na kupokea mpira. Hatua hii inapofikia mpira uwe umemfikia mwezeshaji (aliyeanza kurusha).

Waambie watoto warudie kurushiana mpira wakikumbuka aliyewarushia na wanaowarushia wao.

Endelea na kitendo cha kurushiana ukiwasisitiza watoto wasidondoshe mpira na warushe kwa haraka kadri wanavyoweza.

**Maelezo kwa mwezeshaji:**

Wahamasishe watoto kurusha mpira na siyo kumpa mwingine kwa mkono

Unaweza kuwachangamsha kwa kuwakea muda unatakiwa kupokea na kurusha mpira na kuwaambia wasizidishe muda waliopangikiwa.

Kumbuka kuwahamasisha watoto kadri wanavyoendelea kurushiana mpira ukizingatia kwamba watoto wengine wako taratibu kuliko wengine.

Kama watoto hawawezi kusimama wanaweza kufanya wakiwa wamekaa.

**Utofauti katika mchezo:**

Kitendo hiki kinaweza kutumika kama "mchezo wa majina" kusaidia wanakikundi kujuana majina. Kuwezesha hili, mwambie kila mmoja kutaja jina la mtu anayemrushia mpira.

Kutumia majina inaweza kuwa njia ya kusaidia wanakikundi kuwa makini.

### Sababu za kundi/watoto kufurahia mchezo...

▶ Huu ni mchezo rahisi ambao unachangamsha viungo nya mwili na akili.

▶ Unawafurahisha watoto kwa kushiriki katika kurusha na kudaka wakati huo huo kukumbuka mwenendo wa mchezo.



# Mchezo # 3: Tembea huku na kule

kundi kubwa / umri 3+ / nguvu ya kati-kubwa

**Malengo:**

Kutoa fursa ya kupitia namba, rangi na wanyama wakati huhuo kuwafahamu wanakikundi wengine.

Kuwapa nafasi watoto kufanya shughuli za kutembea tembea na ambazo zinawafurahisha.

**Nia:** Mchezo huu unanatoa fursa ya kuwaunganisha watoto na kuwafanya wawe pamoja kwa furaha. Kwa kutumia dhana za mafunzo kama; numba,rangi na wanyama mwezeshaji ana nafasi ya kupitia pamoja na watoto kwa njia ya ushirikishwaji. Huu mchezo ni mzuri wakati watoto wanapokuwa na nguvu na wanataka kutemebea tembea, hasa wakati wawezeshaji wanapoona watoto hawakai na wamechoka na wanahitaji kufanya kitu kingine.

**Vifaa:** Idadi ya aina mbalimbali zitakazoelezwa na mwezeshaji.

**Hatua kwa hatua:**

Wakusanye watoto na anza kupitia dhana zitakazotumika kwenye mchezo kwa mfano-namba, rangi, wanyama, miezi nk.

Waambie watoto kuanza kutembea tembea wakati ukiimba"tembea huku na kule"

Kadri watoto wanyotembea, waambie waunde makundi kulingana na kundi lao;:

- Makundi ya 2, 3, 5, etc.
- Makundi kulingana na idadi dada/kaka zao
- Makundi kulingana na rangi wanayoipenda
- Makundi kulingana na wanyama wanaowapenda
- Makundi kulingana na tarehe sawa za kuzaliwa
- Makundi kulingana na umri
- Namna yoyote ya kuunda makundi utakayoona inafaa

Baada ya kuunda makunda unaweza kupitia kila kundi na kuwauliza kundi lao linaitwaje. Kwa mfano uliza kila kundi mnyama wanaempenda, wana dada wangapi, wana umri gani.

Wakishamaliza mchezo unaweza kuwaongoza kutoa taarifa fupi;

- Je ilikuwa rahisi au ngumu kutafuta kundi?
- Ulijisikiaje ulipopata kundi?
- Mnajisikiaje mnapokuwa wamoja kati ya watu tofauti tofauti?
- Jadili mifumo inayoweza kusaidia watoto wanapokatishwa tamaa "ya kujumuika na kikundi".

**Maelezo kwa mwezeshaji...**

▶ Ni muhimu kuhakikisha mchezo unafanywa kwa haraka haraka

▶ Unaweza kuwauliza watoto wakusaidie kutambua aina ya makundi

▶ Wakati wa majadadiliano baada ya mchezoi toa nafasi kwa watoto kueleza walivyojisikia wakati wa mchezoi. Jadili namna tunavyojisikia sawa na wao, au tofauti na wengine.Kuwa sawa au tofauti kunaweza kuwa na matokeo ya namna tunavyojisikia.



# Mchezo # 4: Mchezo wa wanyama

kundi kubwa / umri 4+ / nguvu ndogo-kubwa



**Malengo:** Kuwawezesha watoto kufanya shughuli ya kufurahisha ambayo inawafundisha majina na sauti za wanyama mbalimbali.

**Nia:** Shughuli hii inaweza kuwa ni mapitio au zana ya kufundishia kwa dhana mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanyama, rangi, namba idadi (angalia idadi kwa maelezo zaidi).

**Vifaa:** Mpira mdogo or kitu laini kwa ajili ya kurusha.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa mjadala wa kuanisha wanyama (au dhana mbadala kama rangi na namba).

Waulize watoto aina za sauti za wanyama mbalimbali.

Waulize watoto rangi aliyonayo kila mnyama.

Baada ya mapitio kukamilika, wambie watoto wakae kwenye duara.

Chagua wanyama 3-4 (au namba, rangi) kutegemeana na ukubwa wa kundi.

Zunguka duara na chagua mnyama mmoja (au namba/rangi) kwa kila mtoto. Kwa mfano, tembea na chagua: Mbuzi, simba, paka, mbwa, mbuzi, simba, paka, mbwa, etc. mpaka watoto wote wamepewa mnyama (au namba au rangi).

Watoto wakishasimama kwenye duara, ita jina la mnyama mmoja.

Waeleze watoto kwamba wanaposikia majina ya wanyama wao lazima waondoke pale walipo na kwenda kusimama sehemu nyingine kwenye duara. (Kwa mfano ukiita simba, simba wote lazima waondoke walipo na kusimama sehemu nyingine).

Endelea kuita mnyama mmoja baada ya mwingine huku vitendo vikifanyika kwa haraka.

Mara watoto watakapokuwa wameuelewa mchezo vizuri, ita majina mawili kwa wakati mmoja (kwa mfano simba na mbuzi) hii itawafanya watoto wengi kusogea na hivyo kuchamgamsha mchezo.

## Utofauti katika mchezo...

▶ Kama ilivyoelezwa, mchezo huu unaweza kufanyika pia kwa kutumia rangi kuchagua rangi nne: nyekundu, bluu, njano, kijani. Hii inaweza kuwa fursa ya kufundisha rangi kuu na za kawaida.

▶ Mchezo huu unaweza kufanywa kwa kutumia namba. Kwa kundi lenye uelewa mkubwa unaweza kutumia fursa hii kufundisha kujumlisha na kutoa. Kwa mfano kumwita mtoto mwenye namba 2+4 kusogea.

# Mchezo # 5: Chini ya kamba

kundi dogo/kubwa / umri 5+ / nguvu ndogo na kubwa

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto kucheza mchezo wa kusogea kwa pamoja

Kuhamasisha ushirikiano, umoja na mawasiliano.

**Nia:** Ingawa ni rahisi, mchezo huu ni zana muhimu ya kuhamasisha ushirikianao, umoja na mawasiliano katika kikundi. Hakikisha kwamba pamoja na "kufurahishwa" watoto pia waelewe kwamba ni lazima kufanya kazi kwa pamoja ili waweze kufikia lengo la mchezo. Hii ni fursa ya kwaeleza watoto kuhusu uongozi, usikivu, kutatua matizo na umoja.

**Vifaa:** Kamba za kuruka.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wasimame kwenye mstari wakiwa wanangalia kamba.

Kuwe na wawezeshaji wawili watakaoshika kamba (kila mmoja kwenye ncha ya mwisho) zungusha kamba kwa kuruka.

Hakikisha kwamba wawezeshaji wanasimama karibu ili kutengeneza mduara ambao unatosha kwa watoto kuruka.

Anza kuning'iniza kamba taratibu taratibu huku ukiwaeleza watoto kila mmoja kujiandaa kuruka.

Waeleze watoto kwamba ni lazima wawe waangalifu, kuangalia namna kamba inavyotembea isije ikawachapa. Waache waruke mpaka waridhike.

Waambie watoto wasimame wawili wawili.

Kipindi hiki watoto wanatakiwa kupanga pamoja namna ya kuruka kamba kwa pamoja bila kuchapwa na kamba.

Sisitiza kwamba watoto wanatakiwa kutengeneza mkakati wa pamoja (kama vile kuhesabu pamoja kwa sauti au kuwa na ishara kama vile kushikana mikono kama wako tayari kuanza).



**Mchezo huu unafundisha uongozi, kusikiliza, kutatua matatizo na kufanya kazi pamoja!!**

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Waeleze watoto nia ya mchezo.

▶ Fanya mazoezi na wawezeshaji wasaidizi kabla ya kuanza ili uweze kuwaonyesha watoto mfano wa unachotaka wafanye.

▶ Hoji watoto vitu ambavyo vimeufanya mchezo kuonekana mgumu au rahisi. Jumuisha majadiliano kuhusu uongozi, usikivu, utatuaji wa matatizo, na ushirikiano.



# Mchezo # 6: Pitisha Puto

kundi la kati-kundi kubwa / umri 4+ / nguvu ya kati-nguvu kubwa

**Malengo:**

Kuwapa nafasi watoto kucheza mchezo wa kusogea na ambao unawafurahisha.

Kuhamasisha mawasiliano na ushirikiano.

**Nia:** Mawasiliano kwa vitendo ni namna ya mawasiliano ambayo ni muhimu kuendelezwa na kuzingatiwa kadri watoto wanavyokua. Hii ni fursa ya kuwahamasisha watoto kutumia jia zote mbili za mawasiliano kwa vitendo na kwa kuongea ili kufikia lengo la kazi wanayoifanya.

**Vifaa:** Maputo.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wasimame kwenye duara.

Ukiwa umeshikilia puto , anza kwa kutoa maelezo kwamba utampa puto mtu wa kulia kwako ambaye pia atampa anayefuata na kuendelea.

Waeleze watoto kwamba wasirushe puto, ila wampe mtu anayefuata kwa uangalifu, akiwa anamuangalia kuhakikisha anapokea puto vizuri.

Pitisha puto mara kadhaa kuzunguka duara mpaka watoto wote waridhike na wana utayari wa kupokea puto linapopitishwa bila kuliangusha.

Elezea hatua inayofuata ya amchezo: watoto wanaweza kuamua kusogeza alama kwenye duara mara wanapopitisha puto. Wanaweza kusogea sehemu yoyote ya duara na watu wengine itabidi wasogee ili kutoa nafasi na kujaza nafasi iliyotokea. Pitisha puto mara kadhaa kuzunguka duara mpaka watoto waridhike.

Eleza hatua inayofuata ya mchezo: watoto wanaweza kuendelea kufuata mwelekeo mmoja kwa kadri puto linavyopitishwa AU wanaweza kubadilisha mwelekeo. Huu ni wakati muhimu wa watoto kuangaliana na wale wanaotoa na kupokea puto ili kuhakikisha kwamba hakuna nafasi wakati puto linapopitishwa.

Endelea kupitisha puto kwenye duara pamoja na kuzunguka, huku ukiziba nafasi na kubadilisha mwelekeo wa mzunguko.

Wahamasishe watoto kuwasiliana baina yao ili kuziba mapengo, kuangaliana wakati wa kutoa na kupokea puto na kuhakisha kuna uharaka kidogo wa kupokea na kutoa puto.

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Kumbuka kwamba kuzunguka duara kunatokea mara baada ya kupitisha puto. Wambie watoto wazunguke nje ya duara wakati wakiondoa alama kuepuka kugongana au kuzuia mwelekeo wa puto

▶ Anzisha hatua mpya za mchezo iwapo watoto wameshajua na wanafanya vizuri hatua za mchezo wa awali.



## Mchezo # 7: Ingia ndani ya duara

kundi dogo au kubwa / umri 4+ / nguvu ndogo

**Malengo:**

Kuwapa nafasi watoto kupima hisia zao kwa siku hiyo.

Kuanza siku kwa furaha na kwa mchezo wa taratibu.



**Nia:** Ni muhimu kwa wawezeshaji kufahamu nguvu na namna wanakikundi wanavyojisikia kabla ya kuanza michezo/shughuli za siku hiyo. Mchezo huu unatoa nafasi ya kukutana pamoja haraka, kwa urahisi na furaha.

**Vifaa:** Hakuna (i.e. unaweza kuweka kitu kwenye duara).

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae au kusimama kwenye duara.

Anza kwa mfano, halafu waulize watoto kwa kutumia mikono, nyuso, na sauti kuonyesha wanavyojisikia kwa siku hiyo.

Unaweza kuwambia watoto waelezane majina na kama kuna watoto wapya kwenye kundi

Zunguka duara mara 2-3 kuwapa nafasi na fursa watoto kujieleza, kimatendo, kuonyesha, na kujieleza juu ya hisia zao.

**MAELEZO MUHIMU: Kuelezana hisia sio kitu rahisi na ni lazima kufanya kwa umakini ukubwa. Hakikisha unaweka mazingira salama na rafiki ya kubadilishana hisia kwa kuonyesha utayari na kuonyesha mfano wa namna ya kuwasikiliza watoto.**

### Maelezo kwa mwezeshaji...

- Usimlazimishe mtoto kumweleza mwenzake kama hataki. Mara zote wape namna mbadala watoto wasiotaka; kwa mfano wanaweza kusema “pita”au wanaweza kupiga makofi.
- Usipime au kucheka wakati mtoto anapowaeleza wenzake.
- Wahamasishe watoto kutumia sauti au kelele (wasitumie maneno) kueleza hisia zao.



# Mchezo # 8: Imba nyimbo ndefu

kundi dogo-kubwa / umri 2+ / nguvu ndogo au kubwa

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto kucheza mchezo wa kufurahisha ambao unawahamasisha kutumia sauti na miili yao

Kufurahi na kuhusisha fikra za watoto pamoja na nia yao ya kuchunguza mambo.

**Nia:** Pamoja na kwamba ni mchezo rahisi kuimba nyimbo ni namna nzuri ya kuliunganisha kundi.

**Vifaa:** Hakuna

**Hatua kwa hatua:**

Waongoze watoto kuimba.

Kama ni wimbo ambao watoto hawaufahamu, anza kuimba kwanza, halafu ukate kate wimbo huo ili iwe rahisi kuwafundisha na waache warudie rudie mpaka watakapokamilisha wimbo wote.

Endelea kuimba/kuwafundisha watoto mpaka watoto waufahamu wimbo vizuri na kuwa tayari kuimba bila kuongozwa.

**Utofauti katika mchezo:**

Inafaa na ni vema kuwauliza watoto nyimbo gani wanazifahamu na kama wanaweza kuwafundisha wenzao.



**Unaweza kutumia mchezo huu kufundisha kuhusu uongozi!**

**Kwa mfano, unaweza kuwauliza watoto wanaofahamu nyimbo maalumu kuwafundisha wenzao. Au, kama kuna watoto wakubwa kwenye kundi, wambie waongoze wimbo au miondoko inayofuatana na wimbo huo!**

**Maelezo kwa mwezeshaji...**

▶ Chagua wimbo unaoendana na umri na nguvu waliyonayo watoto.

▶ Kwa kadri itakavyowekana, jaribu kuingiza vitendo na staili ya uchezaji ili kuwashirikisha watoto zaidi. Kama una watoto wakumbwa kwenye kundi, wahusishe kwa kuwapa uongozi wa kuongoza nyimbo au vitendo.



# Mchezo # 9: Rafiki nisaidie kutafuta!

wawili wawili (walio kwenye umri sawa) / umri / nguvu ndogo-kati

**Malengo:**

Kuwahamasisha watoto kucheza wawili wawili au zaidi.

Kuwasaidia watoto kubadilishana mawazo.

Kujenga uwezo wa kusikiliza.

Kuwawezesha watoto kuweza kuona vitu kwa mtizamo wa mtu mwingine.

**Nia:** Kusaidia maendeleo ya mtoto na kuhamasisha shughuli zinazohusisha watu wawili wawili (k.m. kufanya shughuli wawili wawili) kuna weza kuwa na faida kubwa. Mchezo huu vile vile ni mzuri kufundisha kuhusu viuongo vitano vya hisia na kuwasaidia watoto kuboresha stadi za mawasiliano (Kusikia, kuongea na lugha ya mwili).

**Vifaa:**

Rangi na vifaa vidogo dogo e.g. vitofali, madoli, sindano za nguo).

Kitambaa cha kufunga uso (sio lazima, ila pale tu kundi litakapokuwa watu wanaofahamiana na kuaminiana).

**Hatua kwa hatua:**

Kabla ya kutambulisha mchezo, wakumbushe/wafundishe watoto kuhusu viungo vitano vya hisia: Kuona, Kunusa, Sauti, gusa na onja. Unaweza kuanza mjadala kwa kusimulia hadithi (kwa mfano, hadithi kuhusu mnyama aliyepoteza kitu wanachokitafuta, au anayekwenda kutafuta chakula, na ambaye anatumia viungo vyake vya hisia kutafuta kitu chake).

Baaada ya kuwakumbusha/fundisha watoto kuhusu viungo vya hisia onyesha mada kwa vitendo kwa kuchora tairi ambalo utaligawa katika vipande vitano na kuandika majina ya viungo katika kila kipande kufuatano na picha yake (kwa mfano sikio kwa ajili ya sauti, mdomo kwa ajili ya kuonja).

Ongoza majadiliano mafupi juu ya namna viungo nyetu vinavyotusaidia katika maisha yetu ya kila siku.

Jadili kwa nini na ni kwa namna gani mawsiliano ni muhimu na vipengele mbalimbali vya mawasiliano (Kusikia, kuongea na lugha ya mwili).

Elezea kwamba watoto watajigawa wawili wawili na kila watu lazima washirkiane pamoja kufikia lengo la mchezo.

Onyesha mchezo kwa kutoa mfano kwa watoto:

- Muulize mwezako (mwezeshaji msaidisi) kufumba macho wakati unaweka kitu (dori au nguo) nyuma ya watoto kwenye ardhi na bila mpangilio.

- Baadae mwambie mwezako afungue macho yake lakini WASIANGALIE nyuma (Badala yake wanaweza kutumia kifunga macho , hii inafanyika tu iwapo kundi linaona kuna usalama katia yao na watoto wanafurahia changamoto ya kutokuona).

- Taratibu muelekeze mwenzako kwenye mwelekeo ulipoweka kitu/kifaa kwa maneno na fununu. Kwa mfano rudi nyuma hatua mbili, hatua tatu kushoto, simama. Sasa rudi nyuma kidogo. Sasa nenda chini, kiko kushoto mwa mguu wako!

Badilisha majukumu na rudia tena.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Hakikisha hakuna vitu vya hatari kwenye eneo la kuchezea ambavyo watoto wanaweza kukanyaga wakati wanatembea.

▶ Sisitiza dhana muhimu na nia y amchezo: Kusikiliza kwa makini na kuongea kwa ufasaha.

▶ Kumbuka kwamba matumizi ya kifunga macho ni mbadala na inafaa tu kama watoto wanajuana vizuri na kuaminiana.



# Mchezo # 10: Changanya, changanya

kundi kubwa / umri 4+ / nguvu ya kati

**Malengo:**

Kuwapa nafasi watoto ya kutembea tembea na kuisisimua miili yao iwe na nguvu.

Kutumia njia ya kujichanganya, kuwafundisha watoto sehemu mbali mbali za mwili (kama mabega, magoti) kwa sababu baadhi ya watoto ni wadogo na wengine inawezekana wasijue Kiswahili.



**Nia:** Mchezo huu ni wa kufurahisha na unachanganyisha watoto na kuweza kutebea tenbea huko wakijichanganya pamoja. Una nia ya kila mmoja kuwa na nguvu na maranyingi huishia na kusheka sana. Unaweza kufanyika ama wakati nguvu ya kundi ni ndogo na wanahitaji msaada au wakati watoto wanapokuwa wamedhoofika na wanahitaji nguvu kidogo kwa kutembea.

**Vifaa:** Hakuna.

**Hatua kwa hatua:**

Waeleze watoto waanze kutembea bila mpangilio.

Anzisha wimbo wa "changanya, changanya, changanya" kadri wanavyotembea.

Katika hali isiyokuwa ya mapangilio wambie "wasimame" katika hatua hii kila mtoto itabidi asimame na mwezake. (hakikisha kwamba watoto wote wana wenzao, kama unafanya na idadi ya namba witiri mwambie mwezeshaji aingie ili kundi liwe na namba shufwa.

Wakiwa wamesimama na wenzao, wambie "waguse" mifupa/sehemu za mwili, ukitaja mifano kama: Kiwiko kwa kiwiko; Goti kwa goti; Mkono kwa mkono; Mgongo kwa mgongo.

Onyesha aina 3 au 4 halafu waambie wajichanganye tena. Rudia kusimamisha katika hatua mbalimbali huku ukitaja viungo mbalimbali.

Namna watoto wanavyozidi kuzoea dhana unaweza kuufanya mchezo kuwa na changamoto, kufurahisha, Au kusisimua kwa kutaja mifano kama : Mkono kichwani; Bega kwa goti; paja na got; kiwikonk.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Kuwa mwangalifu na hali ya kimaumbile ya watoto ili kuhakikisha kwamba hakuna mtoto anayejisikia kuachwa nje ya mchezo.

▶ Onyesha mfano kwa watoto kwa kuwa mchezaji na mshiriki katika mchezo.

▶ Baada ya mchezo, unaweza kufundisha kuhusu sehemu za mwili (hasa kwa watoto wadogo) kwa kupitia sehemu za mwili ambazo zilitajwa wakati wa mchezo.



# Mchezo # 11: Napeleleza kwa jicho langu dogo

kundi kubwa / umri 5+ / nguvu ndogo

**Malengo:**

Watoto kuweza kuzingatia muda na mahali walipo.

Kuwapa watoto changamoto ya kuzingatia mazingira yao.

Kutoa nafasi ya kushirikiana na kuwa pamoja.

Kufundisha watoto rangi na herufi.

**Nia:** Mchezo huu unampa nafasi mwezeshaji kuwaleta watoto kwenye mada ili waweze kuzingatia dhana au mchezo. Vile vile mchezo huu ni mzuri kupitia rangi na herufi.

**Vifaa:** Hakuna.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae pamoja na waangalie mazingira yanayowazunguka.

Angalia mazingira yanayokuzunguka na chagua kitu kimoja utakachokiona. Toa maelezo machache kwa watoto kuhusu kitu ulichokichukua kwa kuwaeleza kwamba "napeleleza na jicho langu dogo kitu flani ambacho ni cha kijani" AU "napeleleza kwa jicho langu dogo kitu ambacho kinaanza na herufi B.

Wape watoto jukumu la kubuni kitu ambacho unaweza kuwa umekichagua.

Kutegemeana na umri wa watoto ulio nao, unaweza ukawapa nafasi ya kubuni mara 3 au 5.

Kama watoto watabuni vitu visivyo na rangi sahihi au wakaanza na rangi sahihi, chukua muda kuwafundisha kuhusu aina ya rangi au herufi ya kitu hicho.



**Huu ni aina ya mchezo wa kubuni! Unasema: "Napeleleza na jicho langu dogo kitu flani ambacho ni..."**

Kama una kundi la watoto wakubwa, na ambalo ni kubwa, unaweza kuligawanya kundi katika sehemu mbili na kuwa na timu mbili za ushindani, wambie timu mojawapo kuchagua kitu na kuwapa timu nyingine nafasi 3-5 kubuni kitu walichochagua.

Timu ikipata jibu sahihi wanapewa alama, na kama watashindwa kubuni, timu inayochagua inapata alama. Endelea kuongeza alama mpaka timu mojawapo ifikie alama 10.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Mchezo huu ni mzuri kwa kupitia rangi na herufi. Tumia ubunifu wa aina yoyote ile ili watoto wajifunze.

▶ Wakati watoto wanapochagua kitu chenye rangi sawa au wameanza na herufi sahihi lakini sio kile ulichochagua hakikisha kwamba unakubaliana na rangi au herufi. Uweza kusema kitu kama "Ndio" ule mwavuli ni wa bluu. Ile ndo rangi sahihi, lakini nina kitu kingine tena kwenye akili yangu. Kitu gani kingine tena chenye rangi ya bluu.



# Mchezo # 12: Wa kwanza kushika

## kundi kubwa / umri 5+ / nguvu ya kati au kubwa

**Malengo:**

Kutumia mchezo wa vitendo ambao utawafanya watoto washiriki na wazingitie kundi lao

Kusaidia kujenga mwasiliano kati ya mikono na macho.

Kutoa fursa kwa wanakikundi kufahamiana zaidi.

**Nia:** Mchezo huu ni mzuri kucheza kama kuna watoto wageni ambao wamejiunga na kikundi kwa kuwa wanapata nafasi ya kujitambulisha. Vile vile unatoa fursa kwa mwezeshaji kujifunza zaidi kuhusu kila mtoto ikiwa ni pamoja na vitu wanavyopendelea, uwezo wao wa kimwili, uelewa wao wa kiswahili, na namna wanavyojisikia wanapokuwa kwenye kundi.

**Vifaa:**

Mpira au kitu laini kwa ajili ya kudaka.

Vifaa vya kuchorea

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae au wasimame kwenye duara (Kulingana na nguvu walionayo).

Anza kwa kurusha mpira kwa watu tofauti tofauti walioko kwenye duara kila mtu akitaja jina lake anapopokea mpira na kurusha mpira kwenda kwa mwingine.

Wakisharusha na kudaka mpira wote na umeshasikia jina la kila mmoja, rusha tena mpira kwa kila mmoja huku ukiwambia waelezane kuhusu mambo yafuatayo: rangi aipendayo; mnyama anayempenda AU ni mnyama gani wangependa wawe kama wangekuwa wanyama; Kinywaji wanachopenda; Chakula wanachopenda; sehemu wanayopenda duniani (unaweza kuwa mji, jiji, nyumba, sehemu ya kutembelea, nk); kitu anachofanya kupteza muda; mtu muhimu kwake; Kitu ambacho ni muhimu kwake.

Baada ya watoto wote kuambiana aina zao, washukuru kwa kuweza kuambiana vitu wanavyovipenda na kwamba umefurahishwa na umeweza kuwafahamu zaidi.

Unaweza kufuatilia mchezo huu kwa kuwapa watoto vifaa vya kuchorea. Usiwaambie wachore kitu gani, waache wachore chochote wanachofikiria.

Kitu wanachochagua watoto kuchora kitamwezesha mwezeshaji kupima na kutambua hisia za watoto au kitu wanachofikiria katika siku. Kwa mfano, mtoto anaweza kuchora mmoja wa wanafamilia anaemfikiria, wengine wanaweza kushora chakula wanachopenda etc.

Pata maelezo kutoka kwa kila mtoto kuhusu alichochora waulize maswali ya kujieleza kuwapa nafasi ya kukwambia wanachofikiria kwa kipindi hicho na wanajisikiaje kuhusiana na kitu hicho.

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Unapofanya kazi na watoto wadogo, una weza kupitia rangi na wanyama haraka haraka kabla ya kuanza mchezo.

▶ Unaweza ukagundua kwamba watoto nao wanataka kueleza vitu ambavyo hawavipendi. Hii ni nzuri sana. Kumbuka kuwa na sehemu muafaka ya kupeana taarifa. Sikiliza kila mtoto na kama inawezekana kaa na kila mmoja na mpe nafasi ya kukueleza mawazo yao na namna wanavyojisikia.

# Mchezo # 13: Sepetu

kundi kubwa / umri 8+ / nguvu kubwa

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto katika mchezo wa kutembea tembea na unaowafurahisha.

Kupitia namba.

**Nia:** Huu ni mchezo wa nguvu unaowapa nafasi watoto kukimbia katika mazingira waliyopo. Unaweza kuchezwa wakati watoto wana nguvu ya kutosha na wanahitaji kutembea tembea. Hata hivyo kwa kuwa ni mchezo wa nguvu ni muhimu kuwa makini na nguvu waliyonayo watoto katika kundi.

**Vifaa:** Mpira.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa kuwambia watoto wasimame kwenye duara.

Mwezeshaji asimame katikati ya duara, wape watoto namba ukiwasisitiza kwamba wasizisahau. Na wewe jipe pia.

Elezea mchezo:

- Mtu aliyeko katikati arushe mpira hewani na aite numba,

- Mtu ambaye namba yake imeitwa lazima adake mpira, wakati wengine wakiendelea kukimbia nje ya duara.

- Mara baada ya kudaka mpira, waseme kwa nguvu 'simama' na watoto wote wasimame.

- Mtu aliyeko katikati atarusha mpira kwa lengo la kumpiga mtu mwingine.

- Kama yule mtu atapigwa na mpira, wote watarudi kwenye duara na mchezo utaanza upya.

- Kama yule mtu hatapigwa na mapira, mtu aliyekuwa anarusha mpira lazima arudishe mpira na asimame katikati.



**Huu ni mchezo unaohitaji nguvu nyingi unaowafanya watoto wasiopenda kukaa kuchangamka! Ila wakumbushe watoto wawe wacheze taratibu...**

Rudia mchezo, kwa kutoa alama kwa kila mtu anayefanikiwa kurusha mpira mpaka mmojawao atakapofikia alama 5 au kumi au mpaka watoto watakapochoka.

## Maelekezo kwa mwezeshaji...

▶ Hakikisha kwamba unawaeleza na kuwafafanulia vizuri wakati wa kurusha mpira wasirushe kwa kuelekeza kichwa, ila walenge kwenye mwili.

▶ Angalia kwa makini kama kuna mtoto mwenye kidondo au uvimbe au sindano kwenye miili yao.

▶ Tumia namba kama fursa ya kujifunza – wasaidie watoto waweze kufurahia mchezo wakati wa kuchagua na kuita namba.



# Mchezo # 14: Nataka cha kwangu...

kundi kubwa / umri 6+ / nguvu ndogo

**Malengo:**

Kuliunganisha kundi kwa mchezo wa kurusha na kudaka mpira.

Kuwashirikisha watoto kwenye mchezo wa ubunifu.

**Nia:** Mchezo huu unawapa nafasi watoto kufikiri kuhusu kitu flani ambacho ni muhimu kwao kwa wakati huu. Inaweza kuwa ni halisi, kufikirika au kitu cha mfano. Kutokana na kwamba watoto wameacha vitu mbalimbali majumbani mwao kabla ya kuja hospitali na kwamba wengi wao wanagawana vitu vyao na wenzao wakati wakiwa wodini, mchezo huu unatoa nafasi kwa watoto kutoa matarajio na matakwa yao kwa namna ya kuwa na kitu cha kwake. Mchezo huu humfanya mwezeshaji kufahamu namna watoto wanavyojisikia

**Vifaa:** mpira.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae au wasimame kwenye duara kulingana na nguvu ya kila mtoto.

Anza kwa kupitisha mpira kwenye duara bila kuchagua mtu (k.m kurusha mpira kwenye duara kwa namna tofauti tofauti) huku kila mtu akitaja jina lake kadri wanavyopokea na kurusha mpira kwa mtu mwingine kwenye duara.

Kila mmoja akisha rusha au kudaka mpira na wamesha taja majina yao wote, rusha tena mpira kuzunguka duara muda huu kwa haraka zaidi.

Baada ya hapo wambie watoto warushiane tena mpira, huku ukiwapa nafasi kukaa na mpira kwa muda. Wakati wakiwa na mpira waulize waelezane kitu ambacho wangetaka kukaa nacho. Kwa mfano "Nataka kubakia na begi langu la shule", "Ningependa kubaki na huu mpira", "Nitapenda kuendelea kuwa na marafiki zangu nitakapoondoka ocean Road", "ningependa kubakia na viburudisho vyangu bila kumpa mtu mwingine!"

Ufanye mchezo uchezeke na wenye kufurahisha, ili watoto waweze kufikiria kwamba wanaweza kuwa na kitu cha kumiliki.

Baada ya kila mtoto kushiriki kurusha na kupokea mpira, pitisha mpira kwenye duara tena kwa haraka zaidi kutoka mtu mmoja kwenda mwingine.

Toa maelezo kwa kikundi baada ya mchezo kwamba ni muhimu kuwa tayari kuacha baadhi ya vitu vyetu au tunaweza tusipate muda wa kutosha kukaa na watu au vitu tunavyovipenda. Tunaweza kukaa lakini wakati mwingine tunaona tunataka kuwa na vitu vyetu wenyewe, ni muhimu kuona umuhimu wa kugawana vitu vyetu na watu wengine.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Huu ni mchezo mfupi unaotumika kugusa hisia za watoto na ufahamu juu ya mawazo yao.

▶ Mchezo ulibuniwa wakati wa ''kurushiana mpira'' wakati mtoto mmoja alipokataa kurusha mpira.



# Mchezo # 15: Kupita kwenye pete mduara

Kundi la kati-kundi kubwa / umri 4+ / nguvu ya kati

**Malengo:**

Kuwashirikisha watoto kwenye mchezo wa kutembea unaowafurahisha.

Kuhamasisha ushirkiano kati ya watoto.



**Nia:** Huu ni mchezo mzuri wa kusaidia na kuleta kundi pamoja. Mchezo wa haraka unaoleta nguvu kwenye kikundi na kukifanya kuwa na furaha bila kuhitaji nguvu nyingi.

**Vifaa:** Pete mduara.

**Hatua kwa hatua:**

Simama kwenye duara pamoja na watoto.

Wambie washikane mikono.

Shika pete mduara mkononi ukiwa umeshikana na mtu anayekufuatia.

Wambie watoto wachezeshe mduara (hoop) na mduara kuzunguka duara kwa kupita kwe pete mduara.

Endelea kuwakumbusha watoto kuwatambua wenzao ambao wana maumivu ili waweze kupitisha mduara pete juu ya mikono yao.

Endelea kuwahamasisha watoto na kuwasaidia kutatua matatizo kadri wanavyopita kwenye pete mduara.

Mchezo uwe wa haraka. Mchezo huu ni kwa ajili ya kuwawezesha watoto kuwa na nguvu, sio lazima kuwa na nguvu nyingi wakati wa kuanza mchezo.

**Maelezo kwa mwezeshaji...**

▶ Mara nyingi watoto wanaweza kuwa na vidonda au sindano kwenye mikono, kiwiko au mikono. Kuwa mwangalifu na kama ikibidi washike pete mduara juu ya maeneo yenye maumivu.

▶ Pamoja na kwamba mchezo huu ni rahisi, ni fursa pekee ya watoto kujifunza na kuwafahamu wenzao wenye vidonda kwa ajili ya kuwasaidia wakati wa kucheza.



# Mchezo # 16: Bata bukini

kundi la kati na kubwa / umri 2-6/ nguvu ya kati au kubwa

**Malengo:**

Kuwashirikisha watoto kwenye mchezo rahisi wa kibwagizo.

Kuwafundisha watoto wadogo (wenye umri 2 - 5) aina mbalimbali za wanyama na sauti zao.

**Azma/Nia:** Wakati unavyofanya kazi na watoto wa shule za awali ni muhimu kuwa na michezo rahisi na jumuishi, hata wakati wa kufundisha dhana na mawazo kama vile Mashamba ya ng'ombe.

**Vifaa:** Hakuna.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae kwenye duara.

Anza kutembea kwa kulizunguka duara kwa nje, taratibu .

Mguse kila mmoja kichwani au begani na kuwaita bata bata.

Bata..."mara nyingi kadri utakavyoweza na baadae umwite mtoto mmoja "bata bukini".

Mtoto anayepewa jina la "bata bukini" atasimama na kukufukuza kuzunguka duara, akijaribu kukukamata kabla hujapata nafasi ya  ya kukaa kwenye duara.

Kama mtoto atakukamata, itabidi ubakie umesimama na urudie hatua za juu. Kama mtoto hatakukamata na ukakaa kwenye duara, itakuwa ni zamu ya mtoto kuzunguka duara na kumwita kila mwan kikundi "bata" or "bata bukini".

Endelea na mchezo ili kila mtoto apate nafasi ya kutembea/kukimbia kuzunguka duara.



**Mchezo huu unaweza kuchezwa Na watoto wenye umri wowote ili kuwapa nafasi ya kutembea, hata hivyo ni mzuri zaidi kwa kundi la watoto wadogo. Kwa mchezo wa kuchekesha jaribu kutumia sauti za wanyama badala ya majina "Bata" na "Bata bukini"! Kutakuwa na vicheko vingi...**

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Mchezo huu unafaa kama una kikundi cha watoto ambao wote wanaweza kukaa, kutembea au kukimbia bila kujisikia vibaya. Usifanye mchezo huu kama kuna watoto wasioweza kutembea au kukimbia.

▶ Unaweza kubadilisha majina ya wanyama yanayotumika ili kuwezesha watoto kushiriki zaidi na kujifunza kuhusu wanyama mbalimbali.



# Mchezo # 17: Nifuate

wawili wawili au kikundi / umri 3+ / nguvu ndogo-kumbwa

**Malengo:**

Kuwashirikisha watoto kwenye mchezo wa kushirikiana na kuchekesha na ambao unasismua mawazo yao na unatoa fursa kueleza hisia zao.

Kujenga umakini wa kundi.

**Nia:** Uhitaji wa nguvu ya utabibu kwa njia ya kucheka ni muhimu katika kufanya kazi na watoto wanaokabiliwa na changamoto mbalimbali. Mchezo huu unatatoa fursa ya kuchangamsha na kufurahia kucheka na kucheza. Vile vile, mchezo huu unatoa fursa ya kuona hisia tofauti na ambazo zinaweza kufuatiwa na kuwauliza watoto namna wanavyojisikia kwa siku hiyo.

**Vifaa:** Hakuna kwa ajili ya mchezo. Vifaa vya sanaa vinaweza kuhitajika kwa ajili ya mchezo unaofuatia.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wasimame wawili wawili wakiwa wanangaliana AU wamwangilie mwezeshaji.

Kuwe na mtu mmoja (ama ni mmoja wa marafiki au kiongozi) kuanza kuchezesha mwili na uso.

Onyesha na elezea kwamba mtoto mwingine (kwenye urafiki) au wototo wengine kwenye kundi lazima wamuigize anayeongoza.

Mhamasishe kiongozi kutumia ishara kubwa, ndogo, ndefu, fupi, duara kali, haraka au ishara za taratibu.

Mhamasishe kiongozi aonyeshe aina mbalimbali za hisia kwa kutumia uso kwa mfano - furaha, masikitiko, hasira, kukasirika, kushangazwa, kushtushwa, etc.

Mwelekeze kiongozi kutumia sauti akiwa anatembea.

Aendelee kucheza.

Hakikisha kwamba unashiriki kwenye mchezo pia, ili kuwafanya watoto wajisikie vizuri kuchecheza na kucheka.

Kama mchezo utafanywa na watu wawili wawili, badilisha viongozi kila baada ya dakika 5 au 10 na rudia mchezo kwa mtoto mmojwapo kuwa kiongozi.

Kama mchezo unafanyika katika kundi kubwa, badilisha viongozi baada ya dakika 5 au 10 kwa kumuomba mtu wa kujitolea kuwa kiongozi wakati wengine wakiigiza na kufuata.

Mchezo huu ni rahisi kuufuatilia kwa mchezo wa kuingia au mchezo wa sanaa, kulingana na hisia tofauti tofauti.

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Unaweza kufuatilia mchezo huu kwa maelezo mafupi kuhusu hisia na namna wavyojisikia mwilini. Kwa mfano, mchezo wa sanaa ya kuchora, au kutengeneza kinyago kuonyesha hisia zao kwa siku hiyo.

▶ Vile vile watoto wanaweza kucheza mchezo mfupi wa kuigiza (Watoto wakubwa) ambapo wanaweza kuonyesha aina mbalimbali za hisia.

# Mchezo # 18: Fikiri kitu

kundi dogo au kubwa / umri 5+ / nguvu ndogo



**Malengo:**

Kuwachunguza na kuwapima watoto nguvu waliyonayo na ushiriki wao.

Kuwahamasisha watoto kufikiria na kuongea juu ya ubunifu walionao.

Kutengeneza mazingira ya kuaminiana ambapo kila wazo litakaribishwa na kuungwa mkono.

**Nia:** Huu ni mchezo rahisi ambao unasaidia kuwahusisha watoto kufikiria na wawezeshaji kufahamu hisia walizonazo watoto kwa wakati huo.

**Vifaa:** Kitu chochote; Kwa mfano, mpira, kanga.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae kwenye duara.

Waeleze watoto kwamba mchezo huu unataka ubunifu na kufikiria

Watambubilishe watoto kitu ulichochagua na mchambue kwa pamoja kitu ulichonacho. Kwa mfano unaweza kuuliza: "hiki kitu kina rangi gani? Vitu gani vingine vyenye rangi kama hii? Hiki kitu kina umbile gani? Ni kigumu au laini?"

Anza kwa kutoa mfano mmoja au miwili kuonyesha yafuatayo: "Hiki ni kitu cha ajabu. Kadiri kinavyozunguka duara, kinabadikika umbile na uonekano wake na kinaweza kuwa namna yoyote utakayotaka kiwe. Kwa mfano, kipande hiki ni ni hereni (onyesha hereni inavyoonekana). Au ni..ni kofia kubwa kwa ajili ya sherehe (Kiweke kwenye kichwa kama vile ni kofia)."

Eleza kwamba utapita kuzunguka "kitu cha miujiza" na wahamasishe watoto kukifikiria, kinaweza kuwa kitu chochote watakachohitaji.

Baadae pitisha hicho kitu na ungalie namna watoto wanavyoweza kufikiria "vitu vya ajabu "kwa kulinganisha na vitu mbalimbali.

Hakikisha kwamba kila mtoto anapata nafasi ya kushika na kuelezea kitu hicho.

## Maelekezo kwa mwezesheji...

► Kumbuka kuwa mbunifu kadri unavyoongoza ushiriki wa mchezo. Iwapo maelezo ya mtoto hayajaeleweka, waulize maswali ya kawaida kuhusu uchaguzi wao kama; ahaa unashikilia parachuti, niambie linafanyaje kazi? Unaweza kutuonyesha namna unavyolitumia?

► Wakati unapotoa mifano, kumbuka kwamba kifaa kinaweza kuwa katika sura yoyote au muundo. Kinaweza kupanuka au kusinyaa. Kinaweza kuwa katika hali ya majimaji au ugumu. Kinaweza kuwa kitu chochote kwa mahitaji ya mtoto.



# Mchezo # 19: Hallo, Kwaheri

kundi kubwa / umri 6+ / nguvu ya kati au kubwa

**Malengo:**

Kutumia mchezo wa kuchekesha na matendo kutambua hisia zinazohusiana na msemo wa hallo kwaheri.

Kuwashirikisha watoto katika mchezo wa kuigiza.

**Nia:** Huu ni mchezo mzuri kuufanya wakati unapokutana na kundi jipya au kundi linaloondoka. Kwa mfano mchezo huu unaweza kutumika siku ya mwisho ya mradi, kutoa fursa kujadili mada ya kwaheri.

**Vifaa:** Hakuna.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa kuwambia watoto watembee huku wakisalimiana kadri wanavyokutana.

Eleza kwamba mchezo huu ni kwa ajili ya kutumia mawazo yako kusalimia watu mbalimbali au viumbe unavyokutana navyo. Waeleze kwamba mara mwezeshaji atakavyoeleza aina ya salaam watoto watumie mawazo yao kuonyesha aina ya mahusiano yanayotambulishwa.

Kadri watoto wanavyotembea bila mpangilio, wambie wasimame, mchague mmojawao na mwambie hallo katika namna zifuatazo: Sema hallo kwa mama; Sema hallo kwa rafiki yako ambaye hamjaonana siku nyingi; sema hallo kwa paka; sema hallo kwa mtu mwenye chakula usoni mwake; sema hallo kwa mwalimu wako; Sema hallo kwa raisi wa Tanzania; Sema hallow kwa ua linaloongea; au mfano wowote unaofikiria…

Wakati huu wambie watoto watembee huku wakisema 'kwa heri' kwa wenzao.

Bila mpangilio wambie watoto wasimame, tafuta mmojawao na mwambie "kwa heri" katika namna zifuatazo: Sema kwa heri kwa rafiki yako; Sema kwa heri kwa simba anayetaka akule; Sema kwa heri kwa mtu ambae hamtaonana tena; na mifano mingine…

Maliza mchezo kwa kichekesho na mfano…

Baada ya kumaliza, toa maelezo mafupi kuhusu mchezo kwa kugusia mada ya Hallo na kwa heri.

Unaweza kuwauliza watoto nani watakaechukua muda mrefu kumuaga, na wanajisikiaje kusema hallo kwa mtu huyo. Unaweza kuwauliza pia kufikiria nani itakuwa vigumu kumwambia kwa heri na watajisikiaje?

**Maelezo kwa mwezeshaji...**

▶ Kumbuka kwamba unapofanya kazi na watoto wenye magonjwa yanayohatarisha maisha yao, ni muhimu kuwa makini na mada ya kusema kwa heri. Kuomboleza, kutengana ni mada zinazohitaji uangalifu sana kwa kuwa zinavuta hisia kali.

▶ Kama una watoto kwenye kundi lako ambao hawawezi kusimama au kutembea, hakikisha kwamba wanakaa sehemu ambayo wataangaliana na wenzao.



# Mchezo # 20: Mtandao wa msaada

## kundi kubwa / umri 5+ / nguvu ya kati

**Malengo:**

Kutoa nafasi kwa watoto kuwakumbuka watu muhimu katika maisha yao wanaowasaidia kwa namna moja au nyingine, na kufikiria namna kila mmoja anavyosaidiwa na watu mbalimabali kama vile; wana familia, marafiki, walimu, madaktari na wanajamii.

Kujisikia mmoja wa kundi kwa kuwaeleza kuhusu mtu wanayemjali wakati huo huo akifikiria maana ya "kuwajali" wengine.

**Nia:** Mchezo huu unawakutanisha na kuwaunganisha wanakikundi na kuwafanya wawe karibu na waweze kusaidiwa na wale wanawazunguka.

**Vifaa:** Sufi au kamba.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa kuwambia watoto wakae kwenye duara.

Anza kwa kutoa mfano na kuelezea mchezo kwa kusema kwamba kamba itawakalisha mahusiano muhimu katika maisha yao.

Anza kwa kushika mwisho wa kamba, toa mfano wa mtu katika maisha yako ambaye ni muhimu sana kwako na elezea kwa nini. Kwa mfano: "Mtu muhimu katika maisha yangu ni mama yangu kwa sababu ananipenda na kunilea. Kila wakati ninapojisikia huzuni ananikumbatia na kuniambia maneno ya kunifariji" au "mtu muhimu katika maisha yangu ni dada yangu, Naela. Ananifanya nifurahi, na kupenda kucheza pamoja. Vilevile ninapokosa usingizi ananisimulia hadithi nzuri" ananijali

Baada ya kutoa mfano wako, endelea kushikilia kamba na rusha kigurudumu kwa mtu aliyeko kwenye duara (Mtu aliyeko mbele yako au mbali na wewe).

Mwelekeze huyo mtu kushikilia sehemu ya kamba na kuwambia wanakikundi mfano wa mtu ambaye ni muhimu kwao. Baada ya hapo mpe mtu mwingine aliyeko kwenye duara sehemu iliyobaki.

Endelea kwa kila mwanakikundi mpaka kila mmoja apate nafasi ya kumuelezea mtu muhimu katika maisha yao. Kufikia hatua hii utakuwa na mfano wa tandabui mbele yako.

Kubali namna kamba na mtandao ulivyoumbika na namna unavyoonyesha, namna kila mmoja wetu alivyo na watu wachache (au wengi) ambao wanatujali na ambao tunaweza kuwategemea kwa msaada.

Fungua mjadala kwenye kundi na angalia kama kila mmoja ana cha kuongeza kabla ya kuondoa mtandao…

### Maelezo ya mwezeshaji...

▶ Huu ni mchezo mzuri kufanya wakati watoto hawana nguvu ya kutosha au nguvu ndogo au unapotaka kutumia fursa hii kuwaunganisha watoto.

▶ Hakikisha kuna usalama wa kutosha kwenye kundi kwa kukubali kwamba baadhi ya watoto wanaweza wasiwe na uhakika ni kitu gani na kwa namna gani wagawane na wenzao. Usilazimishe mtoto kugawana na mwenzake.



# Kazi ya sanaa # 1: Ninachokiita nyumbani

mmoja mmoja au kundi dogo /umri 5+

**Malengo:**

Kujifunza zaidi kuhusu kikundi, kitu gani muhimu kwao, na mawazo yao kuhusu "nyumbani".

Kutoa fursa kwa watoto kubadilishana uzoefu juu ya maswala yanayohusu maisha yao.

**Nia:** Ukweli ni kwamba wakiwa hospitalini, mahusiano ya watoto na nyumbani huwa yanakuwa yamebadilika. Kuwapa nafasi watoto ya kukumbuka mahusiano yao walipokuwa nyumbani, tunatoa nafasi ya kutoa hisia na mawazo yao ambayo yanaweza kutusaidia kujua naman nzuri ya kuwasaidia.

**Vifaa:** Karatasi (Moja kwa kila mtoto) na vifaa vya kuchorea (penseli au chaki za rangi).

**Hatua kwa hatua:**

Mpatie kila mtoto vifaa vya kuchorea na karatasi. Wambie watoto waanze kuchora picha zinazohusiana na nyumbani kwao. Wakumbushe watoto kwamba hakuna mwenye kukosea au aliye sahihi katika kuchora na wanaweza kutunza au kuziharibu picha wanazochora wakitaka.

Wape watoto muda wa kutosha ili wakamilishe kuchora picha zao. Wape muda wa ziada kama muda unakaribia kwisha (kwa mfano "haya watoto nawaongezea dakika 5, kama hautamaliza kuchora picha yako unaweza kuondoka nayo na ukaimalizia baadae").

Wakishamaliza kuchora, wambie wakae kwenye duara wakuangalie wewe.

Anza kwa kuwaonyesha picha yako na wasimulie kuhusu picha uliochora. Simulia kwa sura mbalimbali kwa kutoa maelezo ambayo sio lazima yawe kweli au yanayokuhusu wewe.

Ukishamaliza simulizi yako, wambie watoto wakae wawili wawili au katika kikundi na kila mmoja asimulie picha aliyoichora. Wakumbushe kwamba maelezo sio lazima yawe ya kweli au tukio ambalo limewatokea wenyewe. Inaweza kuwa hadithi.

Wakati watoto wakisimuliana, pitia kila kundi kusikiliza baadhi ya simulizi.

Baaada ya kila mmoja kusimulia, watoto wakae kwenye duara na wambie kila mtoto aweleze wenzake neno moja wakati akizunguka duara. Hii itasaidia kufunga mchezo.

**Maelezo kwa mwezeshaji:**

Kama mtoto anapata ugumu kuelezea simulizi yake, msaidie kwa kutumia picha aliyoichora. Anza kwa kuwauliza swali la wazi kama: "niambie unachokiona unavyoangalia picha uliyochora?" baada ya hapo unaweza kuuliza maswali maalumu kumsaidia mtoto kufikiria.

Mara zote watie moyo watoto kwa kuwaeleza kwamba unatambua namna wanavyosimuliana na unapenda wanachosema. Kwa mfano unaweza kusema, "la, lo Felista. Simulizi yako ilikuwa nzuri sana. Hasa nilipenda sehemu ya msichana aliyepanda juu ya mti. Atakuwa ni msichana jasiri. Asante sana kwa kutusimulia.

**Sababu za watoto kufurahia mchezo huu...**

- Utatoa muda kwa kila mtoto kutafakari.
- Kuwagawanya watoto kwenye vikundi na wenzao inapunguza kazi ya kuelezea kundi kubwa.
- Inatoa fursa kwa mwezeshaji kuwatia moyo watoto na kufahamiana.



# Kazi ya Sanaa # 2: Paka rangi dunia yangu

mmoja mmoja, akifuatiwa na kundi kubwa / umri 4+

**Malengo:**

Kuwapa watoto nafasi ya kufahamu aina za rangi na majina yao.

Kutoa fursa ya kuwatia moyo watoto na fursa nyingine za watoto kufanikiwa.

**Nia:** Kujifunza kuhusu vitu mbalimbali na rangi kunaweza kuwafurahisha watoto na kuwachangamsha iwapo watatumia mawazo yao. Kuwasaidia watoto kwa mjadala (mmoja mmoja au kundi kubwa) kunawajengea watoto kujiamini wakiona wanasikizwa na kutambuliwa na mwezeshaji.

**Vifaa:** Karatasi (Moja kwa kila mtoto), chaki za rangi, flip chati kwa ajili ya (mwezeshaji).

**Hatua kwa hatua:**

Mpe kila mtoto karatasi moja. Zunguka kwenye chumba na mwache kila mtoto achague (bila kuangalia) chaki moja ya rangi kwenye boksi au begi.

Kwa kutoa mfano, waeleze kwamba ni lzima kila mmoja achore vitu ambavyo vina rangi sawa na chaki wanayotumia. Kwa mfano kama watachagua njano wanaweza kuchora jua au ndizi; kama watachagua kahawia watachora ng'ombe au meza nk.

Toa muda wa kutosha kwa kila mtoto kuchora. Wasaidie wengine ambao unaona hawaelewi sawasawa. Watoto wanatapaokuwa na muda wa kutosha, unaweza kuwambia wabadilishane rangi na waendelee kuchora. Hii inawapa nafasi watoto kufahamu rangi mbalimbali.

**Maelezo kwa mwezeshaji:**

Wambie watoto maneno yenye kuwatia moyo kwa kadri wanvyoendelea kuchora hata kama hujui walichochora. Kwa mfano unaweza kusema, "Hii inavutia. Unaweza kuniambia kuhusu kitu ulichochora?" Au "Kazi nzuri sana Hassani. Umechora vitu vingi sana kwa kutumia rangi ya bluu. Unaweza kuniambia vitu vyenye rangi ya bluu unavyoviona kwenye picha ulizochora?"

Wasaidie watoto kadri wanavyoendelea kuchora kwa kuwaambia namna nyingine ya kuchora ili wapanue fikra zao. Kwa mfano, unaweza kusema, "naona umechora jua la njano. Unaweza kufikiria vitu vingine vyenye rangi ya njano?" kama hawawezi kufikiria chochote, unaweza kuwatia moyo kwa kuwapa mfano mdogo. Kwa mfano unaweza kusema "naweza kufikiri kitu kingine ambacho kina rangi ya njano… kinatokea kwenye anga usiku, na vinaweza kuwa vingi kwa wakati mmoja. Unaweza kubuni nichofikiria?"

Katika tukio la mtoto kutaja rangi tofauti na kitu chenyewe (kwa mfano mnajadili vitu vyenye rangi ya bluu na mtoto anasema ni "mti"). Badala ya kuwaambia kwamba "wamekosea", rekebisha kosa kwa kusema kitu ambacho kinamjenga kama, "mti ni mfano mzuri wa kitu ambacho ni cha kijani au kahawia. Majani kwenye mti ni ya kijani na shina ni kahawia. Jaribu kukumbuka kwamba mfano huu wakati tutakapo jadili rangi za kijani au kahawia." Kama umeshajadili rangi hiyo, unaweza kuiongeza kwenye idadi (i.e. Kama umeshajadili rangi ya kijani, unaweza kusema, "mti ni mfano mzuri kwa kitu chenye rangi ya kijani. Ngoja tuongeze kwenye idadi yetu ya vitu vya kijani).

## Sababu za watoto kufurahia mchezo huu…

▶ Huu ni mchezo ambao unachangamsha akili na kujifunza kuhusu rangi. Unatoa muda na nafasi kwa watoto kufanya kazi moja moja na kwa kushirikiana.

▶ Sio muhimu iwapo mtoto hajui kuchora vizuri, ni muhimu wajisikie salama kwenye kundi na kuendelea kuchora. Usiulize maswali yanayokatisha tamaa; km hiki ni kitu gani? Badala yake unaweza kuuliza "kitu gani unachokiona hapa?



# Kazi ya Sanaa # 3: Simulizi

kundi dogo au kubwa / umri 2+

**Malengo:**

Kuwasaidia watoto kutafakari umuhimu wa urafiki na kuwasaidia kuelewa maana ya urafiki kwa uelewa wao.

Kushiriki kwenye mchezo wa kushirikiana na kutengeneza kitu cha mfano kama kundi (ambacho watoto wanaweza kukichagua kama kitu cha kuwakumbusha umuhimu wa urafiki).

**Nia:** Kadri mradi unavyoendelea, watoto wataanza kujenga mahusiano kati yao, lakini kama ilivyo kwaida ya makundi mengi ya watoto, huwa kunakuwa na chanagamoto kati yao. Kutambulisha mada ya urafiki kwao kwa ajili ya kujadili, kunaweza kuwapa nafasi ya kutafakari uzoefu wao juu ya urafiki na kueleza maana yake kwao, na hivyo kuwaunganisha na wengine.

**Vifaa:** Karatasi kubwa, chaki za rangi, rangi and brashi.

**Hatua kwa hatua:**

Chukua karatasi pana na chora maduara makubwa kwenye karatasi, kila duara liwe na kipenyo cha wastani wa 20-30 cm. Chora maduara mbali kidogo ili kutoa nafasi kwa watoto kukaa, kila mtoto awe na duara mbele yake.

Wape watoto chaki za rangi na waambie wachore ndani ya duara, huku wakikumbuka mada na maana ya urafiki. Toa mifano ya vitu ambavyo watoto wanaweza kuamua kuchora ndani ya duara kama vile picha ya rafiki yao.

Wakishamaliza kuchora, pita uwaulize kila moja kusema chochote juu ya kitu alichochora kuhusu urafiki. Baada ya kila mtoto kuelezea picha yake, toa utangulizi wa shughuli inayofuata kwa kueleza kwamba sasa watafanya kazi kwa pamoja kuweka vipande vya urafiki juu ya karatasi kwa pamoja.

Kwa kusaidiana na mwezeshaji mwingine tumia rangi na brashi kupaka rangi picha walizochora watoto moja baada ya nyingine, huku ukiwambia waweke mikono yao kwenye michoro yao, wakiunganisha maduara kwa mikono yao. (Sura ya mikono kukutana pamoja na kuweleta marafiki pamoja). Waachie watoto wachague aina ya rangi wanayotaka kuweka kwenye mikono yao kwa ajili ya kubandika kwenye karatasi. Unaweza kuwauliza watoto aina ya rangi inayohusiana na urafiki.



**Anza kwa simulizi kuhusu urafiki. Hii inafungua mawazo ya watoto na inatoa mifano ya maana ya urafiki.**

Endela kuongeza rangi kwenye karatasi mpaka kundi lione mchoro umekamilika.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Hakikisha kwamba watoto wanashirikiana kwa kadri wanavyoendelea kufanya shughuli kwa pamoja, ukiwaeleza kwamba ushirikiano ni sehemu muhimu sana ya urafiki pamoja na upendo.

▶ Tambua kazi ya kila mtoto na washukuru kwa mchango wao katika kikundi.

▶ Njia nyingine: Unaweza kuandika neno "urafiki" katikati ya karatasi na wambie watoto kupamba na kupaka dunia rangi.



# Kazi ya Sanaa # 4: Kujenga urafiki

kundi kubwa / umri 4+

**Malengo:**

Kuunganisha kundi kwa kucheza mchezo wa kurusha na kudaka mpira.

Watoto kushiriki katika mchezo wa kufikiri.

**Nia:** Mchezo huu unawapa nafasi watoto kufikiria kitu ambacho ni cha muhimu kwao kwa wakati huo. Inaweza kuwa ni kitu cha kweli au cha kufikirika . Kutokana na kwamba watoto wameacha vitu vyao vingi nyumbani wakati wanakuja hospitali itabidi watumie vitu walivyonavyo pamoja na wenzao wakati wakiwa wodini, mchezo huu unatao nafasi kwa watoto kueleza matarajio yao au mahitaji kwa kuwa na kitu binafsi cha kwake. Mchezo huu unaweza kumsaidia mwezeshaji kujua hisia na mawazo waliyonayo watoto.

**Vifaa:** Mpira.

**Hatua kwa hatua:**

Wambie watoto wakae au wasimame katika duara (Kutokana na hali ya mtoto).

Anza kwa kupitisha mpira kwenye duara bila mpangilio (km kurusha mpira katika mwelekeo tofauti tofauti) kila mmoja akitaja jina lake wakati anapokea mpira na kurusha mpira kwa mtu mwingine kwenye duara.

Kila mtoto akishataja jina lake na umesikia majina ya watoto wote rusha tena mpira katika mwelekeo tofauti tofauti, kwa wakati huu iwe haraka inavyowezekana.

Baada ya hapo, wambie watoto wapaeane mpira kuzunguka duara, sasa hivi wape ruhusu ya kukaa na mpira kwa muda. Wakati wakiwa wameshikilia mpira wambie kila mmoja, amweleze mwezake kitu ambacho angependa. Mfano, "Nataka kubaki na begi langu la shule", "Nataka kubaki na mpira huu", "Nataka kubaki la marafiki zangu nitakapoondoka hospitali", "Nataka kubaki na vitafunio vyangu sitaki kumgawia mtu!"

Endeleza mwenendo wa mchezo ili watoto waweze kufikiria kama vile wangekuwa na vitu ambavyo wangebaki navyo.

Watoto wote wakishafikiwa na mpira, pitisha mpira kwenye duara tena kwa haraka kutoka mtu mmoja hadi mwingine.

Jadili na kundi baada ya mchezo, kutafakari kwamba mara nying inatubidi tutoe vitu au tusiwe na muda wa kutosha wa kukutana na watu au vitu tunavyopenda. Tafakari ni kwa namna gani wangejisikia kubaki na kitu flani na ni kweli kwamba wakati mwingine tunahiji kuwa na kitu kwa ajili yetu binafsi, ingawa kuwagawia watu wengine ni muhimu sana.

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Hii inatakiwa iwe ni kazi ya muda mfupi ambayo inatumika kujenga uhusiano kwanza ili kufahamu mawazo yao yalipo.

▶ Mchezo huu mwanzoni ulibuniwa wakati mchezo wa "kupeana mpira" wakati mtoto mmoja alipokataa kupitisha mpira.



# Kazi ya sanaa # 5: Mimi na mkono wangu

## kundi dogo na kubwa / umri 3+

**Malengo:**

Watoto kuweza kutafakari juu ya vitu wanavyofurahia kufanya katika maisha yao na kuwaambia wenzao.

Kuwahamasisha watoto kutumia mawazo yao na kufikiri zaidi kuhusu maisha yao.

Kuongoza kundi kwa kutumia shughuli ya sanaa ambayo itawahusisha watoto wa uwezo na rika mbalimbali.

**Nia:** Kwa kuangalia sehemu za mwili, watoto wataweza kurudisha hisia kwao wenyewe na hivyo kuelekeza nguvu zao katika vitu wanvyovipenda na matakwa yao.

**Vifaa:** Karatasi, chaki za rangi, penseli.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa kugawa karatasi kwa watoto na wambie wachague rangi au penseli wanayotaka.

Wamabie kwamba wataanza kwa kufuatisha umbo na mkono. Hii inaweza kufanyika kwa watu wawili wawili (hasa kama unafanya na watoto wadogo)

Kwa kuonyesha mifano yako mwenyewe waeleze kwamba wataanza kuchora sura za vitu mbalimbali wanavyovipenda ndani ya umbo la mkono na kupaka rangi sehemu ya nje ya mkono kwa rangi wanayoipenda au rangi watayoifananisha na picha ndani ya mkono.

Unapofanya na watoto wadogo ambao inawezakana wasiweze kuchora baadhi ya picha ambazo unaweza kuzitambua, mara zote hakikisha kwamba hupimi uwezo wao wa kuchora, ila angalia zaidi aina ya rangi walizochagua na wasiliana nao kujua kwa nini wamechagua rangi hizo na wanafananisha na kitu gani.

Unaweza kuwauliza watoto au kuwasaidia kuandika majina yao kwenye ukurasa. Hii inaweza kutumika kama kichwa cha habari kwenye mafaili yao. Kama unavifaa vya ziada vya sanaa, unaweza kuvitanbulisha baada ya kumaliza kuchora ili watoto waweze kupendezesha picha zao.

Mara baada ya watoto kumaliza kazi yao, unaweza kumuuliza kila mtoto kuhusu picha au rangi kwenye kurasa zao.

Husisha mawazo ya watoto kwa kuwauliza: "kama mkono wako ungekuwa unaongea ungeongea nini?" Waache watoto wajibu wenyewe na waunge mkono ili kutoa nafasi ya majadiliano zaidi kati "yao wenyewe". Kwa mfano, mtoto anaweza kusema, "mkono wangu unasema kwa heri." Unaweza kufuatilia kwa kuuliza, "unasema kwa heri. Unakwenda wapi? Au ni wewe unaekwenda mahali? Wapi huko? unaenda na nani? Utafikaje unakokwenda? Utaona nini/utafanya nini njiani? Nani/kitu gani kitakuwa kinakusubiri utakapofika unakokwenda?"

**Kumbuka:** Wakati unapohitaji kujua kuhusu picha ya mtoto, uliza swali moja baada ya jingine, ili kumpa nafasi ya kuelewa swali na kulijibu vizuri. Usicheke jibu lolote la mtoto.

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Kuwa mwangalifu na nguvu inayohitajika katika mchezo huu. Usifanye mchezo huu kama una mtoto katika kundi lako ambaye hana mikono au ambaye hawezi kuchora.

▶ Mchezo unaweza kufanyika pia kwa kutumia mguu. Watoto wanaweza kufuatisha nyayo zao na kufikiria maeneo ambayo wangependa kwenda na vitu ambavyo wangependa kuvifahamu (km Mguu wangu utanipeleka... serengeti ambapo nitaona simba na kufukuza twiga).



# Kazi ya sanaa # 6: Kuchora Ndoto

mmoja mmoja au kikundi / umri 5+

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto katika mchezo wa kufikiri na kuwasaidia kutafakari juu ya ndoto zao na matarajio yao ya baadae.

Kuwajengea watoto mawazo ya kujiamini kwa kuwapa majibu mazuri juu ya matarajio yao.



**Nia:** Kuwapa nafasi watoto kutafakari na kusema matarajio yao inaweza kutoa fursa ya kwashirikisha watoto katika mjadala wa namna wanavyoyaona maisha yao yanavyoendelea na nafasi ya kuwasaidia kufikia malengo mbalimbali kwa kadri inavyowezekana. Wakati unafanya kazi na watoto walioka katika mzingira magumu kama – wenye magonjwa hatari, ni muhimu kuwa na huruma na mwangalifu.

**Vifaa:** Karatasi, kalamu za rangi au rangi.

**Hatua kwa hatua:**

Tambulisha dhana ya kuota kuhusu maisha ya baadae (i.e. zingatia matarajio na malengo) kwa namna ya kuchekesha, kama kwa njia ya hadithi, mifano na vitu vya kubuni.

Kama unatumia vitu vya kubuni, hakikisha kwamba watoto wamekaa au wamelala vizuri, anza kwa kuounyesha picha ambazo zinaweza kusaidia "kusafirisha kufikia matarajio yao". Kwa mfano, unaweza kubuni zulia la maajabu ambalo lina uwezo wa kuwepeleka kwenye matarajio yao, mahali na muda wanaotaka kwenda. Unaweza pia kutumia picha ya ndege ambae atawapaisha mpaka wanapokwenda, au mzimu ambao utafanya ndoto zao ziwe kweli. Picha yoyote utakayochagua kuitumia kuwasaidia watoto hakikisha kwamba unailezea ili waweze kuonisha na fikra zao.

Mara watoto wakishaona ndoto/matarajio/lengo/mahitaji, waeleze waonyeshe walichokiona kwa kuchora picha kutumia kalamu za rangi na karatasi.

Kila mtoto akishamaliza kuchora sehemu yake, wape muda wa kutosha kubadilishana walichochora (wanaweza kukuonyesha wewe tu, au kundi zima, kutegemeana na mahusiano yaliyopo na hali ilivyo katika kundi) hali ya ndoto ilivyo. Wanaweza kuamua kukwambia kuhusu picha walizochora, au unaweza kuwambia wakusimulie kuhusu "maisha ya baadae". Simulizi inaweza kuhusisha; sauti, maneno, vitu mbalimbali na hata unaweza kutumia zana na kuyumba kuonyesha namna maisha ya baadae "yatakavyokuwa.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Unaweza kufanya mchezo huu baada ya simulizi kuhusu ndoto/shabaha na kuzifanyia kazi (kutoa nafasi kwa mawazo kuja).

▶ Kuwa makini wakati unaongea na mtoto mmoja mmoja – zingatia ndoto matarajio yao na toa muda wa kutosha kwa kila mtoto kufafanua ndoto yake/matarajio/matakwa. Ni muhimu sana kwa mwezeshaji kuwatia moyo watoto kuwa na nguvu ya kutekeleza ndoto zao – unafanya kazi na watoto ambao maisha yao ni ya hofu.



# Kazi ya Sanaa # 7: Kama ningekuwa mnyama...

mmoja mmoja au kikundi / umri 4+

**Malengo:** Kuwapa fursa watoto kuona na kufikiria ingekuwaje kama wangekuwa katika namna nyingine, wangeonekana katika namna mbalimbali.

**Nia:** Mchezo huu unatoa nafasi kwa watoto kuwa na furaha na kuwaunganisha katika namna mbalimbali za maisha (aina zote za maisha, za ndani na nje), ambazo zinaweza kuwa za kufurahisha /kusisimua/huru. Kuwapa nafasi watoto kufikiria "kuwa kama kitu kingine" tunawapa nafasi kutuambia aina ya maisha ambayo yanaweza kuwa magumu, muhimu or mazuri kwao



**Vifaa:** Karatasi, Kalamu za rangi, penseli au vifaa vingine vya kuchorea, na vifaa vya kuandika kwa watoto wanaoweza kuandika.

**Hatua kwa hatua:**

Mchezo huu unaweza kufanyika baada ya simulizi ambayo itasaidia kuhusisha mawazo ya watoto na kutoa mifano mbalimbali ya wanyama. Ongoza mjadala mfupi kuhusu uwezo na tabia za wanyama mbalimbali, hii itawawezesha watoto kufikiria zaidi wanyama ambao wanaweza kujifananisha nao kwa wakati huu.

Wambie watoto wafikirie na waonyeshe aina ya wanyama ambao wangetaka wawe kama wao. Unaweza kuwaambia wachore au waandike.

Watoto wote wakishamaliza kazi zao, hakikisha kwamba unatoa nafasi kwa kila mtoto kuwambia wenzake (ama na wewe au na kundi zima, kutegemeana na mahusiano na hali ilivyo kwenye kundi).

Unaweza kuwauliza watoto kuongea kuhusu michoro yao/maandishi. Kumbuka kukaa na mchoro na muulize mtoto maswali ambayo yatabaki katika utafakari wake. Hapa ni baadhi ya mifano ya maswali unayoweza kuuliza: Kwa hiyo kama ungekuwa mnyama ungekuwa paka? Ungependa kuwa rangi gani paka? Ungeishi wapi? Unaishi na binadamu au wanyama? Unapokuwa umelala, unapenda kuota kuhusu nini?

Mfano ambao unaweza kukusaidia kufikiri kuhusu huu mchezo: mtoto anaweza kusema angependa kuwa ndege anayeweza kuruka mbali. Kaa na picha ya ndege na msaidie mtoto kufikiria ni wapi ndege angaenda na ni kwa nini?

## Maelezo kwa mwezeshaji...

- Usitafsiri mtoto anachosema – toa nafasi, muda na sehemu muafaka kwa watoto kukueleza maana ya michoro yao.
- Kama utaona kwamba watoto wamesimama na hawataki kuendelea na mchezo, anza kwa kutoa mfano wako kwa kuwapa maelezo kwa nini umechagua aina hiyo ya mnyama.
- Kutegemeana na kundi, unaweza kutumia mchezo kukuongoza katika kipindi cha simulizi.



# Kazi ya sanaa # 8: Nyumba au nyumbani?

kundi kubwa (au hata akiwa mtoto mmoja) / umri 6+

**Malengo:**

Kuwapa watoto muda na fursa ya kutafakari kuhusu "nyumbani" kitu wanachopenda kuhusu nyumbani ina matarajio yao watakaporudi.

Kuwapa fursa ya kutafakari namna wanavyojisikia kuhusu kukaa Hospitali na vitu vizuri wanavyoviona hapa.

**Nia:** Mchezo huu unawawezesha walimu na wawezeshaji kutambulisha mada muhimu - "nyumbani". Tunaelewa ukweli kuhusu baadhi ya watoto walioko Hospitali ya Ocean Road na changamoto ambazo lazima wazikabili kabla ya kurudi nyumbani; hivyo ni muhimu kwetu kutambua kwamba wana mahusiano maalum na nyumbani kwao na hospitali.

**Vifaa:** Karatasi, Kalamu za rangi, vifaa vingine vy akuchorea.

**Hatua kwa hatua:**

Unaweza kuanza na simulizi inayohusu nyumbani au kitu binafsi. Baada ya hapo jadili mambo mbali mbali yanayofanya watu wajisikie "nyumbani" au kujisikia kwamba ni wa mahali flani.

Waulize watoto mambo mbalimbali yanayohusu nyumbani kwao wanayoyapata au wanayoyakosa. Tambua na tafakari kwamba ni changamoto kukaa mbali na nyumbani kwa muda mrefu na wape nafasi ya kujadili na wewe kitu watakachosherekea wakati watakapokwenda nyumbani.

Baadae waulize watoto ni mambo gani katika Hospitali ya Ocean Road wanayoyapenda. Kubaliana kwamba lazima kuna vitu ambavyo ni changamoto ukiwa Ocean Road.

Wambie watoto wajadili hali ya maisha ya Hospitalini – Ocean Road kama wanayapenda au hapana. Wawezeshe kuona kwamba wako kwenye sehemu nzuri.

Sasa wambie watumie vifaa vya kuchorea kuonyesha nyumbani "kitu ninachopenda kuhusu ocean road hospitali".

Michoro ikishakamilika, mpe kila mtoto muda wa kuwaeleza wenzake kuhusu mchoro wake pamoja na wewe (mwezeshaji) au na kundi kubwa. Kama inafaa, wasaidie watoto kuleta pamoja michoro yao na iweke kwenye karatasi kubwa na unaweza kuamua kuibandika mahali.



**Ni ukweli usiopingika kwamba watoto katika hospitali ya Ocean Road mara nyingi wanafunikwa na mawazo kuhusu nyumbani – wengi wanaelezea kukaa muda mrefu bila kurudi nyumbani. Mchezo huu unawakilisha fursa ya kujihusisha na mijadala na tatafakari kuhusu.**

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ It is critical that you stay sensitive to the sharing of the children. While many recognize that staying at ORCI is supportive of their health, they may still have feelings of pain, hurt and resentment for having to stay at ORCI. Given the challenging circumstances of living at the ward, it is very important to acknowledge and be sensitive to whatever thoughts or feelings the children are sharing.



## Kazi ya Sanaa # 9: Karibu mgeni!

mmoja au kundi kubwa / umri 5+

**Malengo:** Kuhusisha mawazo ya watoto kwa kutafakari juu ya ni nani wengependa awatembelee zaidi hospitalini, na ujio huo wangependa uonekanaje na matarajio yao ni nini.

**Nia:** Kumwezesha mwezeshaji kufahamu hali ya akili na hisia za kila mtoto.

**Vifaa:** Karatasi, Kalamu za rangi, penseli au vifaa vingine vya kuchorea.

**Hatua kwa hatua:**

Mchezo huu unaweza kufanyika baada ya simulizi kuhusu "safari", "matarajio", "matakwa", "Kukutana" nk.

Wape watoto karatasi na vifaa vya kuchorea.

Wambie watoto wafikirie kitu (wafumbe macho na waongoze kufanya kitu flani kama inawezekana) kwamba wako nyumbani. Wanamsikia mtu mlangoni na wote wanaenda kumuona. Wana mgeni. Wanamkaribisha mgeni nyumbani kwao na wanakaa pamoja. Mgeni nae anakuja na zawadi alizoleta kwa ajili ya mtoto. Mtoto na mgeni wanafanya kitu pamoja.



Waulize watoto kuonyesha ujio wa mgeni mlangoni, zawadi waliyoleta na /au ni kitu gani wanafanya pamoja.

Toa muda wa kutosha kwa watoto kukamilisha michoro yao.

Chukua muda kukaa na kila mtoto au kutegemeana na kundi, wambie watoto waambizane yafuatayo:

- Nani aliyekuja kututembelea?
- Walileta zawadi gani?
- Kitu gani mtoto na mgeni walifanya pamoja?
- Mlijisikiaje kuwa na mgeni?
- Mtoto atamkaribisha mgeni kukaa?

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Hakikisha kwamba unamsikiliza kila mtoto wakati anaelezea mchoro wake na zingatia yale wanayoongea kwa umakini na onyesha kujali au huruma na hali ilivyo. Kutokana na kwamba watoto wengi wamekuwa nje ya nyumbani kwao kwa muda mrefu kuwa mwangalifu wakati watoto wanatoa simulizi zao.

▶ Kama mtoto hajisikii kutoa simulizi yake usilazimishe. Waache wafahamu kwamba bado wana uhuru wa kuamua kutomwambia mtu wazo lao au hisia zao.



# Kazi ya Sanaa # 10: Kwenda safari

kundi la kati au kubwa / umri 4+

**Malengo:**

Kuhusisha mawazo ya watoto na kutengeneza fursa ya "kuondoka " hosipitali.

Kutumia sanaa katika kutengeneza hadithi na umoja katika kundi.



**Nia:** Mchezo huu unaweza kutumiwa kunyanyua nguvu ya kikundi kwa kuwapa nafasi ya "kuondoka" fursa ya kwenda safari na kuona kitu kipya na tofauti.

**Vifaa:** Karatasi ngumu (Kwa kila mtoto); Mpira mrefu, Kamba; mkasi; picha, Kalamu za rangi.

**Hatua kwa hatua:**

Watoto wote wakae chini, na vifaa mbalimbali kama vilivyoanishwa hapa juu.

Onyesha mfano kwa kuchora picha ya kawaida (kama simba au chui) kwenye karatasi, kwa kutumia umbo la karatasi kama sura. Anza kwa kuchora macho (hakikisha kwamba yako umbali wa kutosha kama yalivyo ya kwako), ongeza pua, mdomo, manyoya, na viungo vingine.

Baaada ya hapo, kwa kutumia penseli, toboa matundu mawili sehemu macho yalipo kwa kukandamiza karatasi.

Kwa kutumia penseli hiyo hiyo hiyo, toboa matundu mawili sehemu ya uso chini kidogo.

Kwa kutumia kipande cha mpira au kamba funga kinyago kwa kupitisha mpira kwenye matundu mawili pande zote mbili za kinyago na kuhifadhi katika sehemu salama.

Wasaidie watoto kutengeneza vinyago vyao wenyewe. Kutegemeana na vifaa ulivyonavyo, unaweza kutengeneza aina mbalimbali za wanyama, na kuongezea vipande mbalimbali kwenye kinyago ili kionekane cha kibunifu zaidi.

Watoto wote wakisha kamilisha vinyago vyao, wambie wavae vinyago vyao na wajaribu kufikiria inakuwaje kuwa kama mnyama. Unaweza kuchagua "kwenda safari", kutembea ndani ya chumba au nje, kupata uzoefu wa "kuwa " wanyama. Kama una kamera, unaweza kuigiza kama mtalii, unapiga picha katika safari na kuwaazima watoto kamera na wenyewe waone uzofu wa safari.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Kuwa makini na uwezo wa watoto kuona unapotengeneza vinyago.

▶ Kama watoto hawana uhakika na namna ya "kuwa" wanyama wanaotaka wambie walie kama wanyama na wajaribu kutembea kama wanyama.

▶ Mchezo mbadala unaweza kuwa ni ule wa kutengeneza vinyago vya sura za binadamu. Hii inaweza kufanyika kama njia ya watoto kuonyesha hisia zao.



# Kazi ya Sanaa # 11: Sehemu sita za visa mkasa

mmoja mmoja halafu kikundi / umri 7-8+

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto na kuwapa nafasi kusimulia visa vyao.

Kutumia sanaa kwa njia ya kufurahisha na ubunifu kufahamu "visa" katika maisha ya watoto.



| | | |
|---|---|---|
| 1. SHUJAA | 2. LENGO | 3. KIKWAZO |
| 4. MSAADA nani/kitu gani saidia | 5. KITENDO kuondoa kikwazo | 6. Hitimisho |

**Lengo:** Wakati wa kusimulia kisa sio lazima kiwe na uhusianao na maisha ya mtoto au "kisa", kuwapa nafasi watoto kusimulia visa vyao ni njia nzuri ya kuzoeana nao wakati ukitafakari fikra zao.

**Vifaa:** Karatasi (moja kila mtoto), vifaa vya kuandikia na kuchorea, vikaragosi au madoli (ziada kwa ajili ya ufuatiliaji).

**Hatua kwa hatua:**

Gawanya karatasi na vifaa vya kuchorea.

Kwa kutumia mfano wa kwako (uliotengeneza kabla) mfano wa visa sita, utambulishe mchezo kama ilivyoonyeshwa kwenye meza upande wa kushoto, chini ya picha ya nyani. <<<<

Mwambie kila au wasaidie watoto kugawanya kurasa zao katika vipande sita.

Kwa kutumia maelekezo yafuatayo, mwambie mtoto achore/aonyeshe dhana halisi katika kila boksi.

Pita kuwaangalia na kuwasaidia watoto, kadri inavyohitajika, wakati wakichora visa vyao kwa mfululilizo uliopangiliwa.

Wakishamaliza kuweka visa vyao kwenye mpangalio, kila mtoto akusimulie kisa chake. Namna nyingine, watoto wakubwa wanaweza kuandika visa vyao kwenye kurasa tofauti – katika hatua hii, wakaribishe kusimulia visa vyao na mwezeshaji au na kundi kama wanataka.

Vile vile, watoto wanaweza kutumia madoli au vikaragosi kusimulia visa vyao kwenye kundi.

## Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Visa mkasa vinaweza kuonyesha kwa kiasi kikubwa hisia alizonazo mtoto; hivyo kama kisa kinamgusa sana mtoto, inaweza kuwa ngumu kumwambia mtu. Usimlazimishe mtoto kueleza kisa chake bila yeye mwenyewe kuwa tayari. Waache waeleze sehemu ya kisa chao wanavyoona inafaa.

▶ Unaweza kuwaauliza watoto wakubwa wanaojua kuandika, kuandika visa vyao, na kusimulia kisa chao katika kikundi au mwezeshaji (namna watakayotaka wao).



# Kazi ya Sanaa # 12: Mti wa familia

mmoja mmoja / umri 6+

**Malengo:**

Kuwahusisha watoto na kazi ya sanaa inayosaidia kufahamu dhana ya familia. (Kuzaliwa na kuchaguliwa) na dhana ya kusaidiana.

Kutumia sanamu au picha kuhusu ulinzi na msaada.

Kujifunza zaidi kuhusu watu muhimu kwa maisha ya watoto.

**Nia:** Mchezo huu unawapa nafasi wawezeshaji kujifunza zaidi kuhusu maisha ya watoto na watu muhimu katika maisha yao. Vile vile, mwezeshaji anaweza kujifunza zaidi kuhusu mahusiano ya watoto, na kuchunguza ni kwa namna gani mtoto anayesaidiwa wakati wa matatizo anavyojisikia.

**Vifaa:** Karatasi (Moja kwa kila mtoto), penseli, Kalamu za rangi au rangi.

**Hatua kwa hatua:**

Gawa vifaa vya kuchorea na karatasi kwa kila mtoto. Elezea kwamba kila mmoja ataonyesha namna familia yao ilivyo (mti wa familia). Eleza vilevile kwamba wanaweza kuchora alama au kuandika namba (na hata kuandika majina).

Wambie waonyeshe kwenye shina la mti. Halafu wambie watengeneze matawi kwenye pande mbili za familia: upande wa baba na mama, kila mmoja na wazaliwa wenzie (ie. Wajomba na mashangazi wa mtoto), mababu, etc. Watoto wanaweza kuonyesha wazaliwa wenzao wanaowafuata chini ya mti. Kila mwana familia anaweza kuonyeshwa kadri mtoto anavyotaka. Wanaweza pia kuamua kuongeza marafiki zao, binamu, au majirani kwenye mti wa familia.

Baada ya kuonyesha kila mwanafamilia, mtoto anaweza kutumia rangi na vifaa vingine vya sanaa kukamilisha picha zao za mti wao wa familia kwa kuchora matawi, maua, majani, nk.

Watoto wote wakishamaliza kuonyesha, unaweza kuamua kuangalia kazi ya kila mtoto, ukiwauliza kama kuna kitu chochote kwenye mti wa familia wangetaka kuwambia wenzao. Vil vile, kama kuna mazingira mazuri katika kundi, watoto wanaweza kuulizwa kama wana kitu chochote katika mti wao wa familia wanaweza kuwasimulia wanakikundi wote.

Kama muda na nguvu inaruhusu, unaweza kumuuliza kila mtoto kama ana kumbukumbu yoyote ya jambo la familia ambalo anaweza kuwasimulia wenzake kwenye kikundi.

**Maelezo kwa mwezeshaji...**

▶ Mada ya mti wa familia na nyumbani ni muhimu kwa watoto wanaokaa mbali na familia zao (Kama ilivyo kwa watoto wa Ocean Road) . Kuwa muangalifu na makini juu ya mada hii na waruhusu watoto kusimilia vitu wanavyotaka wenyewe, usiwalazimishe.

▶ Kama unafanya shughuli hii na watoto wakubwa, unaweza kuwambia waandike historia ya familia zao. Vilevile, unaweza kuwambia waandike herufi kuwakilisha wanafamilia.



# Kazi ya sanaa # 13: Mjumbe mwenye manyoya

mmoja moja / umri 4+

**Malengo:** Kutumia sanaa na kufikiria namna ya kuwapa watoto fursa ya kufikiri salaam ya kuwapelekea wanaowapenda.

**Nia:** Mchezo huu unafaaa wakati unafanya na watoto walioko mbali na kwao (kama walivyo wa ocean road) ambao wana nafasi ndogo kuungana na ndugu zao walioko mbali. Kwa kutumia vitu vinavyoonekana kama ndege, watoto wanaweza kufikiria nje ya maisha wanayoishi na kutuma salaam kwa rafiki au ndugu.

**Vifaa:** Karatasi (moja kila mtoto), kalamu za rangi na rangi.

**Hatua kwa hatua:**

Anza kwa kubuni kitu cha kuonekana au kisa mkasa kuleta mawazo ya watoto kwenye picha ya ndege. Gawa vifaa vya kuchorea na karatasi.

Waeleze kwamba kila mmoja atatumia muda wake kuchora picha ya ndege wake wa ajabu, ambaye ana uwezo wa kuruka popote pale duniani.

Waeleze kwamba huyo ndege ataruka kupeleka salaam kwa yeyote watakaemchagua. Mifano inaweza kua wanafamilia, marafiki, wageni katika nchi nyingine, Malaika, Mungu. Wambie kufikiria vitu kama: ukubwa wa ndege, rangi, mdomo, mkia, manyoya, macho, nk. Mara watoto watakapokuwa na picha kwenye akili zao, wambie waonyeshe ndege wao.

Mara watoto wote watapokuwa wamemaliza kuonyesha ndege wao, unaweza kuangalia picha ya kila mtoto, waulize kama kuna kitu wanataka kusimuliana kuhusu ndege wao. Vile vile kama mazingira ni mazuri, unaweza kuwambia kusimulia kitu chochote na kundi zima kuhusu ndege wao wa ajabu na salaam.



**Mchezo huu wa kufikiri ni wa kibinafsi na unahitaji tahadhari hasa kwa watoto ambao wametengana na familia zao na marafiki. Watoto watakueleza mmoja baada ya mwingine, wanaweza kuwasimulia wenzao kama wataamua kufanya hivyo. Kuwa mwangalifu na kumtia moyo kila mtoto kwa picha na maneno aliyoandika.**

### Maelezo kwa mwezeshaji...

▶ Watoto wanaoishi mbali na familia zao na marafiki zao (Kama walivyo watoto wa Ocean Road) wanaweza kujisikia vibaya kupeleka salaam. Kuwa mwangalifu na makini, waache watoto wasimulie vitu wanavyotaka wao. Usiwalizimishe kusimulia kama hawataki.

▶ Kwa kufuatilia, kama unafanya na watoto wakubwa, unaweza kuwaambia waandike salaam zao nyuma ya picha zao, katika namna ya maneno mafupi au barua.

Children in Crossfire

2 St. Josephs Avenue, Derry / Londonderry
BT48 6TH Northern Ireland
+44 (0)28 7126 9898

P.O. Box 23204
Dar es Salaam, Tanzania
+255 (0)22 277 5965

**infotz@childrenincrossfire.org**
**www.childrenincrossfire.org**